Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00065 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Mei 15-21, 2024 |

# Samia: Nishati safi ya kupikia itawakwamua wanawake kiuchumi



Zaidi ya Waafrika milioni **900** wanatumia nishati isiyo safi ya kupikia

Uk. 4

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akihutubia viongozi mbalimbali, wadau wa nishati pamoja na washiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika uliofanyika katika Makao Makuu ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (Unesco) jijini Paris, Ufaransa jana. Rais Dk. Samia pia ni Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano huo wa Kimataifa ambao umewakutanisha viongozi kutoka sehemu mbalimbali duniani.

KITAIFA Uk. 5

## SMZ yawakalia kooni wakala wa elimu ya nje wababaishaji



HITILAFU YA INTANETI:

## Ubalozi wa Marekani wafungwa kwa siku mbili

Na Mwandishi Wetu

UBALOZI wa Marekani nchini Tanzania, umefungwa kwa siku mbili kutokana na ukosefu wa mtandao wa intaneti iliyoathiri nchi kadhaa za Afrika Mashariki. Uk. 2

AFYA Uk. 7-8

## Fahamu dalili za magonjwa manane ya figo



SIASA Uk.12-13

## 'Dikteta' Mbowe anavyomwonea wivu, husuda Rais Samia



BAJETI YA MIFUGO, UVUVI 2024/2025:

## Ndege 85 zisizo na rubani kudhibiti uvuvi haramu Uk. 4



100 km kwa saa 2

Kasi ya kusafiri ndege hizo zikiwa zinachukua picha za kiwango cha juu

## Waziri Mkuu aiahidi Unicef kuendeleza ushirikiano Uk. 2

# Majaliwa aiahidi Unicef ushirikiano



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Mkurugenzi Mkazi wa Unicef, Elke Wisch, ofisini kwake Bungeni jijini Dodoma jana.

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameliahidi Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) kuwa Serikali ya Tanzania itaendelea kulipa ushirikiano ili liendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika sekta mbalimbali zikiwemo za elimu, afya na maji.

Majaliwa alitoa ahadi hiyo jana baada ya kukutana na Mkurugenzi Mkazi wa Unicef, Elke Wisch, ofisini kwa Waziri Mkuu Bungeni jijini Dodoma jana.

Katika mazungumzo yao Mheshimiwa Waziri Mkuu amemuahidi Bi. Wisch kuwa Serikali ya Tanzania itaendelea kulipa ushirikiano Shirika hilo ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika sekta mbalimbali zikiwemo afya, maji na elimu.

Kwa upande wake, Wisch aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuweka mipango katika kuboresha sekta ya elimu, mpango wa kukabiliana na maafa pamoja na kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Aidha, Wisch aliahidi kuwa Unicef itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzamia katika kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa kukabiliana na maafa.

## MABADILIKO YA TABIANCHI:

# AF yatakiwa kuendelea `kuipiga jeki' Tanzania

> Mkutano huo uliwashirikisha watendaji na watalaamu wa serikali na Sekretarieti ya AF ambapo pamoja na mambo mengine, utaainisha maeneo maalum ya kipaumbele.

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu, Mhandisi Cyprian Luhemeja, ameutaka Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (AF), kuendelea kuipatia Tanzania fedha za kuendelea kutekeleza miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi inayotekelezwa maeneo mbalimbali nchini.

Mhandisi Luhemeja alitoa wito huo alipokuwa akifungua Mkutano wa kubadilishana uzoefu kwa nchi wanachama zinazotekeleza miradi inayosimamiwa na AF jijini Dodoma juzi.

Mkutano huo uliwashirikisha watendaji na watalaamu wa serikali na Sekretarieti ya AF ambapo pamoja na mambo mengine, utaainisha maeneo maalum ya kipaumbele na mikakati mbadala ya kusaidia kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mhandisi Luhemeja aliushukuru Mfuko huo kwa kuipatia fedha Tanzania na kuahidi serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, itahakikisha fedha zinazotolewa zitaendelea kuelekezwa katika miradi ya kipaumbele iliyoanishwa na AF hasa ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Aliongeza kuwa ajenda ya mazingira ni moja ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita na kutokana na umuhimu huo, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kusimamia vyema miradi inayolenga kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi iliyotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini ili kuzisadia jamii.

Alisema kutokana na umuhimu wa ajenda ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi Mazingira (Nemc) limeialika Sekretarieti ya Mfuko huo pamoja na Nchi Wanachama kuja Tanzania ili kujifunza majukumu, mafanikio na changamoto inazopitia Nemc kuona miradi inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini inavyoweza kukabiliana na madhara ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa vitendo.

Mhandisi Luhemeja alisema mkutano huo baina ya Nemc na Mfuko huo, utasaidia kupatikana njia mbadala za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo uchimbaji wa visima vya maji, mbinu za kisasa za umwagiliaji mashambani, ufugaji wa kisasa na jinsi mbinu hizo zinavyoweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa maeneo husika.

Alisema Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa wito kwa jamii kutunza na kuhifadhi mazingira ikiwemo kujenga utamaduni wa kupanda miti.

Naye Mratibu wa Mfuko huo, Farayi Madziwa, aliipongeza Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa juhudi mbalimbali inazoendelea kuzifanya katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Alisema fuko huo utaendelea kutoa fedha na kujenga uwezo wa kitaalamu kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## UCHAGUZI MDOGO KWAHANI:

# Tume yawafunda watendaji

**Na Mwandishi Wetu**

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi, imewataka watendaji wa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Kwahani, Zanzibar, kutekeleza wajibu na majukumu waliyopewa kwa kuzingatia katiba, sheria, kanuni na miongozo iliyotolewa na itakayotolewa na Tume wakati wa uchaguzi mdogo.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji mstaafu Jacobs Mwambegele, wakati akifungua mafunzo kwa mratibu wa uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo.

Mafunzo hayo yalianza juzi na yanatarajiwa kuhitimishwa leo Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Jaji Mwambegele alisema uchaguzi ni mchakato unaojumuisha hatua na taratibu mbalimbali za kisheria zinazopaswa kufuatwa na kuzingatiwa kwani hatua na taratibu hizo ndiyo msingi wa uchaguzi kuwa mzuri, wenye ufanisi na hivyo kupunguza au kuondoa malalamiko ama vurugu wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.

"Nachukua nafasi hii kuwaasa kuwa pamoja na uzoefu ambao baadhi yenu mnao katika uendeshaji wa uchaguzi, mhakikishe mnazingatia maelekezo mtakayopewa na Tume badala ya kufanya kazi kwa mazoea. Hivyo, itafaa zaidi tutakapohitimisha mafunzo yetu hapa, sote tuwe na utimamu wa kusimamia uchaguzi kwa ufanisi wa hali ya juu badala ya uzoefu," alisisitiza Jaji Mwambegele.

Sambamba na kuzingatia sheria, Jaji Mwambegele aliwakumbusha washiriki wa mafunzo na kuwasisitiza kuwa, wakati wote wa mchakato wa uchaguzi, ni vema wakavishirikisha kwa karibu vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi kuhusu masuala ya kiuchaguzi wanayostahili kushirikishwa, kwani jambo hilo litawarahisishia utekelezaji wa majukumu.

Aliongeza kuwa ni muhimu kwa watendaji hao wa uchaguzi pia, kuhakikisha wanalitambua na kulijua vyema eneo ambalo uchaguzi utaendeshwa ikiwemo miundombinu ya kufika katika vituo vya kupigia kura.

Kadhalika, Jaji Mwambegele aliwasisitiza kufanya utambuzi na kukagua vituo vya kupigia kura mapema ili kubaini mahitaji maalum ya vituo husika kwa lengo la kuhakikisha mpangilio mzuri ambao utaruhusu uchaguzi kufanyika kwa utulivu na amani.

"Kuhakikisha mnaajiri watendaji wa vituo wenye weledi, wanaojitambua na tuachane na upendeleo kwa ndugu na jamaa ambao hawana sifa za kufanya shughuli za uchaguzi," alisema na kuongeza:

"Kuhakiki vifaa vya uchaguzi mnavyopokea kutoka Tume na kuhakikisha kila mkuu wa kituo anapata vifaa vyote vya uchaguzi vinavyohitajika mapema; kuvipatia vyama vya siasa orodha ya vituo vya kupigia kura ili kuviwezesha kupanga mawakala."

Vilevile, aliwataka wahakikishe siku ya uchaguzi wanaweka utaratibu utakaowezesha kila kituo cha kupigia kura kufunguliwa saa 1:00 asubuhi; na kufanya mawasiliano na Tume pale ambapo utahitajika ushauri kuhusiana na masuala ya uchaguzi.

"Mmeaminiwa na kuteuliwa kwa sababu mnao uwezo wa kufanya kazi ya kusimamia uchaguzi, hivyo jambo muhimu mnalotakiwa kuzingatia ni kujiamini na kufanya kazi kwa weledi," alisema

Mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi yemelenga kuwakumbushamambo muhimu kuhusu usimamizi, uratibu na uendeshaji wa uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Kwahani Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Ratiba ya uchaguzi huo inaonesha kwamba, fomu za uteuzi wa wagombea zitaanza kutolewa kuanzia Mei 17 hadi 23, mwaka huu uteuzi ni Mei 23 na kampeni za uchaguzi zitaanza Mei 18 hadi Juni 7, mwaka huu na uchaguzi utakuwa Juni 8, mwaka huu.



Jaji mstaafu Jacobs Mwambegele

## HITILAFU YA INTANETI:

### Ubalozi wa Marekani wafungwa kwa siku mbili

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa Marekani nchini Tanzania, umefungwa kwa siku mbili kutokana na ukosefu wa mtandao wa intaneti iliyoathiri nchi kadhaa za Afrika Mashariki.

"Kwa sababu ya huduma duni za mtandao kote nchini, Ubalozi hautafunguliwa kwa umma," Ubalozi ulisema kwenye chapisho kwenye X (zamani Twitter) juzi Jumatatu.

Ubalozi huo umeahirisha miadi yote ya konsula kwa siku ya jana Jumanne na leo Jumatano hadi mambo yatakapotengamaa.

Ubalozi huo, hata hivyo, utaendelea kupatikana kwa makusanyo ya visa na kushughulikia kesi za dharura zinazohusisha raia wa Marekani.

Mtandao uliyopotea tangu Jumapili asubuhi, umesababisha umeathiri huduma za intaneti nchini Tanzania, Kenya, Rwanda na Uganda.

Tathmini ya kampuni ya ufuatiliaji wa mtandao ya NetBlocks siku ya Jumatatu ilionyesha kuwa Tanzania imeathirika zaidi na kukatika kwa huduma za intaneti.

Hitilafu hiyo imetokana na kukatika kwa nyaya za chini ya bahari zinazounganisha eneo hilo na dunia nzima kupitia Afrika Kusini, mtaalam wa sekta hiyo Ben Roberts aliambia BBC.

Siku ya Jumatatu, watu katika mataifa ya Afrika Mashariki, walikuwa bado wanafikia kiasi kidogo sana cha mtandao huku baadhi ya watoa huduma za mawasiliano wakionyesha kuwa suala hilo lilikuwa bado halijatatuliwa kikamilifu. BBC.



Sehemu ya majengo ya Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Njombe.

Viongozi, Wadau wa Nishati pamoja na Washiriki mbalimbali, wakiwa kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika uliofanyika katika Makao Makuu ya Unesco jijini Paris, Ufaransa jana.

# Dk. Samia: Nishati safi ya kupikia itawakwamua wanawake kiuchumi




**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema licha ya Afrika kuwa na idadi kubwa ya watu na raslimali zote muhimu, ni bara la chini kuwa na upatikanaji wa nishati safi ya kupikia.

Zaidi ya Waafrika milioni 900, wanatumia nishati isiyo safi ya kupikia, jambo ambalo linachangia uharibifu wa mazingira, upotevu wa bioanuai na athari za kiafya.

Rais Dk. Samia aliyasema hayo akiwa Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano Mkuu wa Nishati Safi ya Kupikia uliowakutanisha Marais, Viongozi na Wadau mbalimbali wa Afrika katika Makao Makuu ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) jijini Paris, Ufaransa jana.

Rais Dk. Samia alisema nishati safi ya kupikia ina maeneo matatu.

La kwanza alilitaja kjuwa ni hasa maeneo ya vijijini ni uwezo mdogo kutokana na gharama kubwa na upatikanaji wake pia ni taabu.

La pili alisema ni ulimwengu kwa jumla kutolipa suala hilo kipaumbele. Ufadhili mdogo na watu kutokujua fursa za kiuchumi zilizopo kwenye nishati safi ya kupikia inayorejesha nyuma harakati hizo.

Na pia kutokuwepo ushirikiano wa kuhakikisha nishati safi ya kupikia inapatikana kwa wote. Rais Samia alisisitiza upatikanaji, gharama ndogo na suluhu zinazotekelezeka.

Rais Dk.Samia pia alisema kuongezeka kwa upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, itasaidia wanawake kupata fursa zaidi kushiriki shughuli nyingine za kiuchumi, kupunguza umaskini na usawa wa kijinsia.

Hata hivyo, Rais Dk. Samia ambaye pia ni kinara wa kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, Afrika,

Alisema licha ya changamoto hizo, Tanzania ina dhamira ya kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia uliozinduliwa hivi karibuni uliokusudia kufikia asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia nishati hiyo ifikapo mwaka 2034.

Aliwaeleza wajumbe wa Mkutano huo uliohudhuriwa na zaidi ya watu 1,000 wakiwemo Marais, Viongozi mbalimbali, asasi za kiraia na wadau masuala ya nishati safi kuwa malengo hasa ni kuhakikisha mbali na Afrika kupata uelewa, lakini pia liwe jambo la kimataifa ambapo pia itakuwa rahisi kuchangia ili kutekeleza azma hiyo.

"Pia nia ni kuandaa sera madhubuti inayotekelezeka kwa ajili ya nishati safi ya kupikia na kuharakisha ushirikiano wa wadau katika suala hilo," alisema.

Inakadiriwa kuwa Dola bilioni nne za Marekani zinahitajika kwa ajili ya matumizi ya Nishati safi bafrani Afrika.

Mwishoni mwa mwaka jana, Rais Dk. Samia alizindua Programu ya Nishati Safi ya Kupikia ya Kusaidia Wanawake Barani Afrika ambayo ilipokelewa vema na viongozi mbalimbali wa bara hilo.

---

## BAJETI YA MIFUGO, UVUVI 2024/2025:

# Ndege 85 zisizo na rubani kudhibiti uvuvi haramu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amemaliza kadhia ya uvuvi haramu nchini kwa kutekeleza mikakati ya muda mfupi na mrefu.

Waziri Ulega alitoa kauli hiyo jana wakati akiomba Bunge kuidhinisha makadirio na mapato na matumizi ya wizara yake ya Sh. bilioni 460.333 kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 jijini Dodoma jana.

"Tunakusudia tuandike historia ya Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais shupavu wa Awamu ya Sita kwa kumaliza kadhia ya uvuvi haramu kwa kuweka na kutekeleza mikakati madhubuti ya muda mfupi na mrefu... Mkakati mmojawapo ni kutumia teknolojia za kisasa ambazo pamoja na kudhibiti, zitazuia uhalifu wa uvuvi katika bahari na maziwa yetu" alisema na kuongeza:

"Teknolojia hizo ni kama vile matumizi ya ndege maalum zisizokuwa na rubani 85 ambazo zina uwezo wa kusafiri kilomita 100 kwa muda wa saa mbili na kuchukua picha za kiwango cha juu za uhalifu wa uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi."

Pia alisema wizara yake inakusudia kuanza kutumia mfumo wa ufuatiliaji wa kielektroniki ambao utafungwa katika vyombo vyote vya uvuvi zikiwemo boti za kisasa zilizotolewa hivi karibuni.

"Mfumo huo utafuatilia mienendo yote ya wavuvi nchini ikiwemo kuweka kumbukumbu za wavuvi. Pamoja na kuzuia uvuvi haramu, mfumo huu utasaidia kuweka usalama wa wavuvi na wananchi ambao wanapata matatizo wakiwa maeneo ya maji."

Alisema teknolojia hiyo itaongeza ufanisi na kupunguza matumizi ya rasilimali fedha na muda.

Aidha, Waziri Ulega alisema wizara yake ina mkakati wa kuongeza uzalishaji, masoko pamoja na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi.

Alisema wizara yake pamoja na mambo mengine, imepanga kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi, kuhamasisha uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi na kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika sekta za mifugo na uvuvi.

Alisema miradi mwingine, itakamilisha kuundwa kwa chombo maalum



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega**

kitakachosimamia uendelezaji wa mazao na miundombinu ya mifugo na mageuzi katika Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (T-CSDTP) wa miaka mitano (5) wenye kunufaisha walengwa 58,000.

"Mradi huo utahusisha kununua ng'ombe wa maziwa 17,200, kujenga mabanda 5,000 ya ng'ombe, kujenga mfumo wa uvunaji maji ya mvua katika kaya 22,400, kununua na kusanikisha mitambo 2,800 ya biogesi, kujenga vituo 950 vya kukusanya maziwa, kununua dozi 929,000 za chanjo za mifugo na kujenga kilomita 140 za barabara," alisema na kuongeza:

"Tutaanzisha kambi moja ya mifugo (Livestock Guest house) katika Ranchi ya Mkata, tutanunua na kusambaza madume 60 ya mbari bora za mifugo aina ya Brahman ili kuongeza uzalishaji na tija katika mnyororo wa thamani wa mifugo na mazao yake."

Miradi mingine kwa mjibu wa Waziri Ulega ni kujenga kituo cha mafunzo ya wadau wa mnyororo wa thamani wa malisho aina ya mabingobingo (Juncao), kuboresha na kuendeleza hekta 20,000 za maeneo ya malisho katika eneo la Msomera, Kitwai na Saunyi.

"Wizara yangu ina mkakati wa kukamilisha ujenzi wa mabwawa saba na visima virefu vitatu, kuwezesha uendeshaji wa mashamba ya kuzalisha malisho na mbegu za malisho na kuwezesha kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia," alisema.

# SMZ yawakalia kooni wakala wa elimu ya nje wababaishaji

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imesema itaendesha msako na kuzifutia usajili wa wakala wa elimu ya nje ambao wanafanya kazi zao kwa ubabaishaji na kuipongeza Global Education Link GEL kwa mchango mkubwa inaotoa kwenye sekta ya elimu.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, alipotembelea ofisi za Global Education Link (GEL) zilizoko katika jengo la Thabit Kombo Zanzibar.

Alisema wizara inatambua kazi nzuri zinazofaanywa na baadhi ya wakala kama GEL, lakini kuna taaasisi zimeingia kwenye fani hiyo na kufanya kazi kwa ubabaishaji, hali ambayo imesababisha malalamiko mengi.

“ Wizara inatambua mchango wa Global Education Link na tunakupongeza tunajua mchango wake kwenye sekta ya elimu, mimi najua nilishawahi kuja kwenye moja ya shughuli zako nikajionea ukubwa wa kazi zenu, lakini wale ambao hawako makini, tutawafutia usajili,” alisema.


Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein

Alisema kuna vijana nchini wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa wakirubuniwa na baadhi ya mawakala wa mfukoni wasio waaminifu, hali ambayo imesababisha malalamiko mengi.

“Nitatembelea wakala wote na wale ambao hawatambuliki, watafunga ofisi, lakini GEL tumejiridhisha mnafanyakazi kubwa sana na kwa kweli nimevutiwa na mawazo uliyotushauri kuhusu namna ya kuwasafirisha wanafunzi wengi nje ya nchi kwa kozi ambazo hazipo hapa nchini,” alisema na kuongeza:

“Mollel tuletee taarifa rasmi kuhusu wazo lako nitaelekeza ofisi yangu iratibu suala hili na kutushauri kwa sababu Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi ni mwelewa sana anataka mabadiliko ameifanya elimu kuwa kipaumbele kwenye serikali yake, siamini kwamba tukimpa wazo hili atalikataa.”

Alisema Chuo Kikuu Zanzibar (SUZA), kinac hangamoto kubwa ya nafasi kwani uwezo wake ni kuchukua wanafunzi 60 kwenye kozi ya afya wakati wanaoomba kozi hiyo huwa ni zaidi ya 800.

“Tunashindiwa kuwachukua kwa sababu hatuna pa kuwaweka na kwa maana hiyo tunakosa wataalamu wengi wa sekta ya afya na kwa hiyo kuna umuhimu wa kuwapeleka nje ya nchi ili tupate wataalamu wengi wa fani ya afya,” alisema.

Naibu Waziri alisema Rais Dk. Hussein Mwinyi anatoa nafasi za vijana kwenda kusoma nje ya nchi, kwa hiyo ni wakati mwafaka kwenda kumshauri kuwapeleka nje wale ambao wanakosa nafasi kwenye fani wanazoomba hapa nchini.

“Elimu ambayo nimeipata ndani ya saa moja hapa ni kubwa sana naomba tuendelee kutoa elimu watu wajue wakitaka kwenda kusoma nje ya nchi wafanye nini, serikali tusijifungie tunatakiwa kukutana na wadau wa sekta binafsi kama Global tunapata mawazo mapya,” alisema.

“Wizara tuko tayari kuratibu mikutano ya mara kwa mara baina ya wadau wa serikali na wa sekta binafsi tupeane mawazo mapya, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao tuwape elimu wajue mawakala wa elimu ya juu wanafanya nini, Global Education Link anafanya nini, maana wasipoelimishwa wanaweza kudhani ni wale wale wajanja wajanja tu,” alisema.

Alisema hivi karibuni Baraza la Wawakilishi litaanza vikao vyake, hivyo atatumia nafasi yake kuitambulisha Global kwa Wajumbe wa Baraza ili wawafahamu na wawatumie kwa ajili ya kupeleka watoto wao nje.

Alisema ingawa GEL ni ya muda mrefu, lakini kuna umuhimu wa kukutana na wadau wengi mara kwa mara na kuwaeleza wanachofanya ili kufautisha na zile taasisi ambazo zimekuwa zikifanya kazi kwa ujanja ujanja.

“Tutakaa na Bodi ya Mikopo, namimi nitaratibu kikao hicho tuone namna ya kusaidia wanafunzi, tumefungua chuo cha Tehama Zanzibar na nia ni kupokea wanafunzi wa kigeni kwa hiyo ni fursa kwenu kuleta wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali,” alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa GEL, Abdulmalik Mollel, alisema wamezungumza mambo mbalimbali na Naibu Waziri ikiwemo namna ya kuitumia elimu kuakisi uchumi.

Alisema Rais Dk. Hussein Mwinyi amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha uwekezaji kwenye uchumi wa buluu na maono makubwa ya kukuza uchumi wa Zanzibar, hivyo kuna umuhimu wa kufanya maandalizi mazuri ya rasilimali watu.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

HII NI KERO



## Umeme bado unakatika

Baada ya kukaa miezi kadhaa nchi ikishuhudia mgawo wa umeme, hivi karibuni tuliambiwa kwamba sasa nchi yetu inazalisha umeme wa kutosha na mgawo haupo tena.

Lakini maeneo mengi ya Dar es Salaam, ikiwemo Temeke Kwa Maganga umeme unaendelea kukatika mara kwa mara. Hata juzi, katika baadhi ya mitaa kwenye eneo hilo hadi asubuhi yake kwa maan aya jana kulikuwa hakuna umeme.

Kinachoonekana huenda umeme sasa unakatika kutokana na hitilafu za hapa na pale lakini wahusika wanachelewa sana kuja kurekeisha hata wakipigiwa simu kupitia call centre. Ni vyema wahusika wafanyie kazi hili. Umeme ni maendeleo.



MAONI YA MHARIRI

# Hatua ya kutumia ndege kukamata wavuvi haramu imekaa vyema

Katika juhudi za kuimarisha ulinzi katika maeneo ya uvuvi, Serikali imesema sasa imekusudia kununua ndege zisizo na rubani (drones) sita zitakazotumika kuangalia wahalifu kwenye maeneo ya uvuvi.

Hayo yalisemwa jana Bungeni na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega wakati akihitimisha hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Uvuvi haramu na usiofuata kanuni umekuwa ni sumu kubwa ya uzalishaji wa samaki kwa njia ya asili kwa maana ya kutegemea bahari, maziwa na mito.

Uvuvi huu usio endelevu, licha ya kupunguza upatikanaji wa samaki, umesababisha jamii ambazo zimekuwa zikiishi kwa kutegemea samaki kuwa katika hali mbaya kiuchumi.

Ni kutokana na uvuvi haramu umesababisha hadi Ziwa Tanganyika kufungwa kwa kipindi cha miezi mitatu ili kuruhusu samaki kuzaliana. Ziwa hilo pengine tangu limeumbwa na Mungu halijawahi kufikia hatua kama hiyo.

Tunafahamu, kwa kipindi kirefu serikali imekuwa ikijitahidi kupambana na uvuvi haramu ukiwa ni pamoja na kuweka doria za mara kwa mara.

Doria kama zilizofanyika katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria miqmwishoni zilisaidia kupunguza vitendo vya uvuvi haramu, biashara ya samaki wachanga na utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi kwa asilimia 80.

Iliwahi kuelezwa kwamba katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2017/2018 - 2019/2020, Kikosi Kazi kilifanya doria na operesheni katika maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Ziwa Victoria na kwa utekelezaji wa doria hizo uliwezesha kukamatwa kwa zana haramu zilizokuwa zikitumika katika shughuli za uvuvi ikiwemo nyavu za makila, makokoro, nyavu za timba (Monofilament) na nyavu za dagaa. Pia, vifaa vilivyokuwa vinatumika kwenye uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi ikiwemo injini za boti pamoja na gari.

Hatua ya kutumia drones kupambana na uvuvi haramu sambamba na kuendelezwa kwa doria za vikosi kazi ibila shaka itasaidia sana kudhibiti uvuvi haramu na pia kuangalia usalama katika bahari zetu maziwa na mito.


Lakini pia tunaishauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa wavuvi ili kuondokana na matumizi ya zana haramu ambazo zinatishia kupungua kwa samaki katika maji ya asili.

Ni vyema pia kwa wavuvi, wafanyabiashara na jamii kwa ujumla kutoiachia serikali katika kupambana na kudhibiti uvuvi haramu. Haya yawe mapambano ya kila mtu.

Lakini kutokana na ongezeko la watu, juhudi pia ziendelezwe za wananchi kufuga samaki kwa kutumia vizimba, mabwawa na hata madumu ili kupunguza utegemezi wa vyanzo vya asili katika kupata samaki.


## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |

Na Hamisi Kibari

JICHO LANGU

# Iko wapi demokrasia ndani ya chama cha demokrasia?

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kipo katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa ndani, baada ya kumaliza kupata safu za viongozi wa ngazi ya chini, hivi sasa wapo katika hatua ya kupitisha majina ya watakaowania nyadhifa za ngazi ya Kanda kabla ya ile ya juu kabisa ya uenyekiti.

Wakati tukitarajia demokrasia kutamalaki katika chaguzi hizi kama lilivyo jina la chama chao, badala yake tunashuhudia malumbano yasiyo na tija wala kwisha miongoni mwa viongozi wa chama hiki!

Makundi katika chaguzi zozote ni jambo la kawaida na ni sehemu ya demokrasia, lakini yakivuka mipaka na kuzua uhasama, chuki na mitafaruku miongoni mwa viongozi wa juu wa chama hii haikubaliki.

Makamu Mwenyekiti wa Chama, Tundu Lissu anasema chaguzi zao zimegubikwa na rushwa iliyokithiri, mwenyewe anasema kuna fedha chafu kutoka kambi ya Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe alizozitawanya kwa wagombea anaowataka ili wazitumie 'kuwalainisha' wapigakura.

Kauli hii ya Lissu imechukuliwa na wafuasi wa Mbowe kama ina lengo la kumchafua Mwenyekiti wao ili Makamu huyo wa Chadema ajisafishie njia ya kushika hatamu ya kuongoza chama hiki kikuu cha upinzani.

Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema ambaye ni 'Timu Mbowe', ameibuka na kumshangaa Lissu kwa kuonyesha dhamira ya kuutaka uenyekiti wa chama chao kinyume na ahadi yake ya huko nyuma!

Lema anadaia Lissu baada ya kusaidiwa na kuuguzwa kwa karibu na Mbowe alipopata madhila ya kupigwa risasi na kunusurika kuuawa, eti aliweka ahadi ya kwamba, hatogombea nafasi yoyote ya uongozi ndani ya chama hicho ambayo Mwenyekiti wake ataonesha nia ya kugombea!

> **Lissu baada ya kusaidiwa na kuuguzwa kwa karibu na Mbowe alipopata madhila ya kupigwa risasi na kunusurika kuuawa, eti aliweka ahadi ya kwamba, hatogombea nafasi yoyote ya uongozi ndani ya chama hicho ambayo Mwenyekiti wake ataonesha nia ya kugombea!**

Kabla hatujakaa vizuri, wiki hii tena ameibuka mwanachama mwandamizi wa Chadema, Halima Mdee na kudai Lissu ana roho mbaya na uchu wa madaraka na anautaka Uenyekiti wa Chama hicho kwa gharama yoyote ile hata kwa kuchafua wenzake!

Mdee ambaye hatambuliki ndani ya Chadema kama mwanachama wao, anaonekana naye anajikomba kwa Mbowe kwa kumchafua Lissu akidhania labda anaweza kupata huruma wa bosi wake huyo.

Sisi wadau wa masuala ya siasa tunajiuliza ile demokrasia inayoimbwa na Chadema siku zote ipo wapi? Kama ndani ya chama chao kidogo wanashindwa kuelewana, wataongoza vipi taifa hili kama watafanikiwa kushika dola?

Malumbano yao haya ni kwa faida ya nani? Kundi la viongozi waandamizi wanapomwandama kiongozi wao mmoja anayekemea rushwa ndani ya chama chao ni kwa maslahi ya nani?

Hivi kuna baadhi ya viongozi ndani ya Chadema nafasi zao wamezikatia hatimiliki na ni marufuku kuguswa na wengine? Kama ndiyo, ipo wapi hiyo demokrasia wanayoiimba huku kwenye majukwaa ya maandamano?

# Fahamu dalili za magonjwa manane ya figo



KWA mujibu wa utafiti wa hivi karibuni wa Shirika la India la Nephrology, watu milioni 84 duniani kote wanaugua magonjwa mbalimbali ya figo. Hii inamaanisha kwamba, mtu mmoja kati ya kila watu 10 duniani, ana aina fulani ya ugonjwa wa figo.

Ikumbukwe kwamba kati ya sababu 10 za vifo duniani, ugonjwa wa figo uko katika nafasi ya saba.

Moja ya sababu za kuongezeka kwa magonjwa ya figo ni kwamba magonjwa haya hayazingatiwi kuwa mabaya katika hatua za mwanzo.

Dk.Milli Mathew, ambaye ni Mkuu wa Hospitali ya MGM Health Care, anasema mara nyingi umakini huoneshwa kwa ugonjwa wa figo ugonjwa huo unapofikia hatua mbaya.

Kwa hiyo, ni muhimu kuelewa magonjwa ya figo na dalili zake na kumsaidia daktari katika hatua za mwanzo za ugonjwa huo.

### Jinsi figo zinavyofanya kazi

Figo ni moja ya viungo muhimu vya mwili wa binadamu, ambayo kazi yake kuu ni kuondoa taka kutoka mwilini kwa njia ya mkojo.

Kwa kusudi hili, figo hutenganisha vitu kutoka kwenye damu, ambavyo ni hatari kwa mwili wa binadamu, ikiwa ni pamoja na baadhi ya madini yasiyo ya lazima na kisha damu safi huzunguka mwilini.

Mtindo wa maisha, lishe, tabia, matatizo ya kijeni, dawa na matatizo mengine yanayohusiana na afya, yanaweza kusababisha figo kushindwa kufanya kazi.

Usumbufu katika utendaji wa kawaida wa figo, husababishwa na magonjwa fulani.


Hatari kubwa katika suala hili ni kwamba ugonjwa huo haujatambuliwa katika hatua za mwanzo na baadhi ya dalili zake hazionekani.

Dk. Milli Mathew anasema, kadiri ugonjwa unavyoendelea, dalili huonekana na unaweza kuelewa maendeleo haya kupitia uchunguzi na vipimo vya afya pekee.

### Magonjwa ya kawaida ya figo na dalili zake

#### Ugonjwa sugu wa figo

Aina hii ya ugonjwa wa figo, hudumu kwa muda mrefu na mara nyingi huwapata watu





wenye kisukari au shinikizo la damu.

Katika hatua za mwanzo za ugonjwa huu, hakuna dalili zinazoweza kuonekana, lakini jambo muhimu ni kwamba ugonjwa huu unaweza kuponywa kwa matibabu sahihi.

#### Dalili

. Kukosa hamu ya kula
. Kuvimba miguu na viungo
. Matatizo ya kupumua
. Kukosa usingizi
. Kujisaidia haja ndogo kidogo.

#### Mawe ya figo

Mawe ya figo kimsingi ni madini ambayo hujilimbikiza kwenye figo na kuwa na muonekano wa mawe.

Kwa mujibu wa wataalamu wa matibabu, baada ya jiwe moja au mawili kuundwa, kwa mara ya kwanza hakuna dalili na mgonjwa hana matatizo yoyote makubwa.

Tatizo hili husababishwa na unywaji wa maji kidogo, unene kupita kiasi, lishe isiyofaa na mtindo wa maisha.

Watu wanaougua ugonjwa

>>>Inaendelea Uk. 8

# Fahamu dalili za magonjwa manane ya figo

>>>Inatoka Uk. 7

huu, hupata shida kupata haja ndogo au kuwa na damu kwenye mkojo. Watu walioathirika hulalamika kwa maumivu kwenye eneo la figo lenye jiwe.

**Ugonjwa wa figo kutokana na kisukari**

Kwa mujibu wa utafiti, kila mtu mmoja kati ya watatu mwenye kisukari, huugua ugonjwa wa figo na figo zao kushindwa kufanya kazi.

Ugonjwa huu ni wa kawaida zaidi kwa watu ambao hawana udhibiti wa ugonjwa wa kisukari.

**Dalili**

. Maumivu ya mguu
. Uchovu
. Kupoteza uzito
.Upele wa mwili
Kutapika.

**Ugumu wa figo na shinikizo la damu**

Mbali na ugonjwa wa kisukari, ugonjwa unaoharibu figo ni shinikizo la damu, kutokana na mishipa ya damu kwenye figo kuharibika na kazi yake ya kawaida huathirika.

Kwa sababu hii, figo haiwezi kufanya kazi yake ya kusafisha vitu visivyohitajika kutoka kwenye damu na haiwezi kuondoa madini hatari kwenye mwili kutoka kwenye damu.

Kwa hivyo, vitu visivyo vya lazima hujilimbikiza kwenye mishipa ya damu na shinikizo la damu huongezeka zaidi.



**"Mbali na ugonjwa wa kisukari, ugonjwa unaoharibu figo ni shinikizo la damu, kutokana na mishipa ya damu kwenye figo kuharibika na kazi yake ya kawaida huathirika. Kwa sababu hii, figo haiwezi kufanya kazi yake ya kusafisha vitu visivyohitajika kutoka kwenye damu na haiwezi kuondoa madini hatari kwenye mwili kutoka kwenye damu.**

**Dalili:**

- Kichefuchefu na kutapika
- Uudhaifu
- Maumivu ya kichwa na shingo.

**Maambukizi katika njia ya mkojo**

Ingawa maambukizi ya mfumo wa mkojo siyo ugonjwa wa figo moja kwa moja, huathiri figo.

Ugonjwa huu unaweza kusababishwa na bakteria na iwapo bakteria hao hawatazuiliwa na kutibiwa haraka, wanaweza kufika sehemu ya juu ya njia ya mkojo na kuharibu figo.

**Dalili:**

- Maumivu ya mgongo
- Homa
- Haja ndogo yenye maumivu
- Maumivu ya tumbo
- Damu kwenye mkojo
- Kuumwa miguu
- Kutapika.

**Ugonjwa wa figo wa polycystic**

Ugonjwa huu husababishwa na uvimbe kwenye kibofu ambao hukua kwa muda na kusababisha figo kushindwa kufanya kazi. Jeni pia inaweza kuwa sababu.

**Dalili:**

- Maumivu katika sehemu ya juu ya tumbo
- Maumivu upande mmoja wa tumbo
- Damu kwenye mkojo au bakteria.

**AJ Nephropathy**

Ugonjwa wa figo kwa kawaida huanza utotoni na wakati wa ujana.

Dk. Milli Mathew anasema, katika ugonjwa huu, kuna damu kwenye mkojo. Ugonjwa huu unaweza kutambuliwa kupitia vipimo.





**Figo kushindwa kufanya kazi**

Katika kushindwa, figo huacha kufanya kazi, kwa sababu mara nyingi, dalili huonekana kwa watu wenye ugonjwa huu, wakati ugonjwa huo unaendelea sana.

Kuna hatua tano za ugonjwa huu na dalili hazionekani hadi hatua ya nne.

Dalili za ugonjwa huu huonekana tu wakati figo zinaacha kufanya kazi kabisa.

**Dalili hizo ni:**

- Kupoteza hamu ya kula
- Kutapika
- Udhaifu mkubwa wa kimwili
- Uvimbe wa sehemu za mwili
- Usingizi. BBC.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Mei 15-21, 2024 |




Jarida hili haliuzwi

# 'Dikteta' Mbowe anavyomwonea wivu, husuda Rais Samia

UK. 12 & 13



# Halmashauri zioneshe mfano utekelezaji maagizo ya viongozi

**Na John Ngunge**

BILA shaka si mara yako ya kwanza kusikia kauli za amri za kupiga marufuku jambo fulani au kutendeka kwa kitu fulani zikitolewa na viongozi.

Marufuku na kauli hizo zimekuwa zikitolewa mara kwa mara kwa nyakati na mazingira tofauti, iwe kisiasa, kidini au kiutawala na nadhalika.

Mara nyingi amri hizo au wakati mwingine kauli za serikali husikika kwenye mikutano ya siasa au mikutano na waandishi wa habari. Kauli za serikali hutolewa pia bungeni ikiwa ni ishara ya kuweka msimamo wa jambo fulani.

Mara kadhaa tumeshuhudia amri zinazotolewa na viongozi, hususan, kwenye mikutano ya hadhara iwe ya kisiasa au mingine, maagizo yao yakipuuzwa kutekelezwa na viongozi wa chini.

Ni katika muktadha huo, Mei 15, 2023, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alikemea baadhi ya watumishi wa umma kudharau maagizo yanayotolewa na viongozi wao.

Alitoa kemeo hilo wakati alipokwenda kuwasikiliza wafanyabiashara wa Kariakoo ambao waligoma kufanya biashara wakipinga kile walichokiita unyanyasaji uliokuwa ukifanywa na watumishi wa Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) katika makusanyo ya kodi.

Kikubwa walikuwa wakilalamikia kamatakamata iliyokuwa ikifanywa na watumishi wa taasisi hiyo ya kodi dhidi yao.

Waziri Mkuu Majaliwa baada ya kuwasikiliza alisitisha Kikosi Kazi kilichoundwa kwa ajili ya kukusanya kodi katika eneo.

Pamoja na hatua aliyochukua, Waziri Mkuu Majaliwa alionesha dhahiri kukerwa na tabia ya watumishi wa mamlaka hiyo kuacha kutekeleza maagizo yanayotolewa na viongozi wakidai kuwa ni ya kisiasa.

"Hakuna mtumishi wa Serikali anayepaswa kumdharau kiongozi wake wa juu," alinukuliwa kusema na kuwataja viongozi hao kuwa ni Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu.

Alipigilia msumari kwenye jeneza akisema chochote kitakachotamkwa na viongozi hao ni agizo nan linapaswa kutekelezwa.

Alisema Rais anapotoa agizo wao kama wasaidizi wake wanapaswa kulitekeleza na si vinginevyo.

"Rais Samia aliagiza madai ya kodi ya miaka mitano nyuma kwa wafanyabiashara, wasidaiwe; lakini TRA wanawaambia watoe barua kuhusu suala hilo. Mnadai barua kwa watu wa Kariakoo, wanapatia wapi barua ya Rais, halafu mnasema agizo lililotolewa na Rais ni la kisiasa, hiyo ni dharau, na natamani nimjue huyo mtu aliyesema hivyo nishughulike naye mara moja," alikuja juu.

Waziri Mkuu Majaliwa alitoa kauli hiyo baada ya wafanyabiashara hao kusisitiza kugoma licha ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati huo, Amos Makalla (sasa hivi Katibu Mwenezi wa CCM) kuwataka kuusitisha, wakisema wakifungua biashara zao Kikosi Kazi hicho kitahitaji



wafanyabiashara hao watoe waraka unaowataka kusitisha mambo yote yanayolalamikiwa.

Walidai kuwa wataambiwa maagizo hayo ni ya kisiasa na hayana ushahidi wa kimaandishi au waraka.

Lakini jambo muhimu la kukumbuka hapa ni kwamba dharau za watendaji juu ya kauli zinazotolewa na viongozi wa juu zimekuwa siyo jambo geni kusikika.

Tuchukue kwa mfano, wakati wa uongozi wa awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais Dk. John Pombe Magufuli (sasa marehemu), ulipiga marufuku halmashauri zote kutoza mazao ya wakulima wanayosafirisha kutoka mashambani kwenda majumbani kwao.

Mfano kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Munduli, unaweza kutusaidia kupata tafsiri ya maana ya mazao. Kwa mujibu wa sheria ndogondogo ya halmashauri hiyo, 'mazao' maana yake ni mazao ya chakula, biashara, maua, matunda na mboga yanayolimwa ndani ya halmashauri.

Na 'mifugo' maana yake ni wanyama wote wafugwao na binadamu na itajumuisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, punda, kuku na bata.

Halmashauri zote zina sheria ndogondogo ambazo ndani yake zimeweka sheria ya kutoza ushuru wa mazao. Sheria hizo zimetungwa na kupitishwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri husika.

Hayati Magufuli kwa nyakati na mahali tofauti enzi za uhai wake alikuwa akisikika kupiga marufuku utozaji wa ushuru wa mazao ya wakulima kutoka mashambani hadi majumbani kwao na hasa mazao yasiyofikia tani moja.

Aliwapiga marufuku wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri au watendaji wa vijiji kuwatoza wakulima ushuru wa mazao, akisema atakayefanya hivyo atakiona cha mtema kuni.

Bila shaka agizo hilo lilitekelezwa, licha ya halmashauri hizo kuwa na sheria ndogondogo zilizoruhusu utozaji ushuru wa mazao hayo.

Baada ya kifo cha Rais Dk. Magufuli, halmashauri nyingi zilirejesha utaratibu wa kutoza ushuru mazao ya wakulima wanayoyabeba kutoka shambani ili kwenda kuyahifadhi majumbani kwao utadhani agizo hilo lilishafutwa!

Kilichofuata baada ya hapo ni malalamiko. Malalamiko yakaanza kusikika kila upande, wakilalamikia ushuru huo. Lakini wiki iliyopita, Watanzania wamesikia tena kauli ya aina hiyo ikitolewa na kiongozi bungeni.

Safari hii aliyetoa kauli ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, kauli ambayo kimsingi siyo mpya na inakwenda kwa taasisi zilezile.

Ni katika Mkutano wa Bunge la Bajeti unaoendelea mjini Dodoma, ndipo malalamiko dhidi ya halmashauri kutoza ushuru wa mazao ya wakulima yaliibuka.

Ilikuwa katika kipindi cha maswali na majibu bungeni, wakati akijibu swali la Mbunge wa Jimbo la Kilombero, Abubakar Damian Asenga, aliibua malalamiko ya wananchi wa jimbo lake na kuhoji: Kwanini wananchi wa Wilaya ya Kilombero wanatozwa ushuru wa mazao chini ya tani moja katika mageti ya Idete, Kivukoni na Kidatu kinyume na maelekezo ya Serikali.

Naye Mbunge wa Jimbo la Bukene, Selemani Zedi, kupitia swali lake la nyongeza aliwasilisha malalamiko ya wapiga kura wake. Zedi aliitaka Serikali kutoa katazo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega Vijijini kuwatoza kodi ya mazao wakulima wa kawaida katika halmashauri hiyo.

Ndipon Naibu Waziri, Dk. Dugange akawaelekeza wataalamu na wasimamizi wa mageti katika halmashauri zote kuacha kutoza ushuru wakulima wanaosafirisha mazao chini ya tani moja ndani ya Halmashauri husika.

Pia aliwataka kufuata utaratibu wa kiwango cha tozo kisichozidi asilimia tatu ya mazao yaliyo chini ya tani moja kwenda nje halmashauri.

Kwa upande wa sheria ndogondogo zinazotungwa na halmashauri, ni kama vile Waziri Waziri Mkuu Majaliwa amepigilia msumari. Ametaka mamlaka husika na hapa ni halmashauri kuacha kupitisha sheria ndogo ndogo zinazowaumiza wananchi.

Waziri Mkuu anasema badhi ya sheria ndogondogo zinazoumiza wananchi zinahawamasisha pia kuwachukia viongozi na serikali yao.

Alitoa angalizo hilo wakati akizungumza na wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa akiwataka kusimamia mapendekezo ya Tume ya Haki ya Jinai iliyoundwa na Rais Dk. Samia.

Ingawa warsha ilikuwa mahususi kwa ajili ya kupewa maelekezo ya kusimammia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki ya Jinai, lakini nadhani imekuwa ya faida kwao ili wasimamie sheria zingine ndogondogo ambazo zimekuwa kero kwa wananchi.

Malalamiko yaliyowasilishwa bungeni na wabunge Asenga na Zedi ambao kwa muundo wa Baraza la Madiwani wao ni wajumbe, yalipaswa kutatuliwa huko katika mabaraza kwa kuacha kupitisha sheria zinazotoza ushuru wa mazao ya wakulima au kuzifuta kama tayari zilikuwepo.

Ushiriki wao katika mabaraza hayo ungesaidia kuondoa kero kama hiyo na nyingine zinazofanana nazo.

Hivi karibuni, Waziri wa Tamisemi, Mohamed Mchengerwa alizitaka halmashauri zote kuibua miradi mingi ya kuziingizia fedha kuliko kutegemea zaidi tozo ambazo alisema nyingi zinaelekezwa kwenye huduma na ruzuku kutoka serikali kuu.

Alisema halmashauri sasa hazitakuwa zinapimwa kwa kufikia malengo ya makusanyo waliojiwekea kwa mwaka ambapo nyingine hujiwekea malengo kiduchu ili mwisho wa siku zionekane zimezidi lengo, bali sasa zitapimwa kwa ubunifu wa wingi vyanzo vipya vya mapato.

Halmashauri nyingi zina ardhi, zina wataalamu na zinakopesheka kwa maana zina uhakika wa kupata mitaji. Pamoja na kuwa na wataalamu zina uwezo hata kwenda kujifunza kwa wengine namna ya kuzalisha kitu fulani kwa tija hata nje ya nchi.

Kwa maana hiyo hazina matatizo ya kuanzisha miradi ikiwemo viwanda vidogo vya kuongeza mnyonyoro wa thamani mazao ya wakulima na wafugaji badala ya kung'ang'ania kuwakamua fedha baada ya kuzalisha mazao yao kwa jasho lao.

Unaweza kukuta halmashauri ya wilaya fulani ina wafugaji lukuki wa ng'ombe lakini inashindwa hata kuanzisha kiwanda kidogo cha kusindika mazao yatokanayo na maziwa na kugeuka kuwa soko la wafugaji au hata kuanzisha kiwanda cha kusindika nyama kama si ngozi na mazao yake!

Halmashauri zibadilike.



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Nyerere alivyotabiri kuja kwa watu wasiotumia *common sense*

"Tusiingie kwenye mtego wa kujenga chuki. Katika nchi yetu, Rais anaweza kutoka popote. Anaweza kutoka Kigoma au Lindi. Anaweza akatoka Wete au Pwani. Anaweza kutoka Tanganyika (Tanzania Bara) au Zanzibar. Tunachopaswa kufanya ni kuhakikisha kwamba pande zote za Muungano ziwe zinajiona zinatendewa haki. Pande zote za Muungano zinaonekana kwa usawa wake kwa sababu hizi ni nchi mbili huru zilizoungana. Na pande zote za muungano ziwe zinaheshimu kila upande."

Maneno hayo yamezungumzwa na Zitto Kabwe na mimi nimeyachukua kutoka kwenye kipande kimoja cha klipu inayozunguka mtandaoni ambapo mwanasiasa hiyo alikuwa akizungumza kwenye mkutano mmoja wa hadhara hivi karibuni.

Zitto anaendelea kusema: "Siyo mmoja aone hawa wachache hawa wengi. Kwenye sheria za kimataifa hakuna nchi ndogo. Seychelles (Ushelisheli) ina watu laki moja, lakini kwenye Umoja wa Mataifa, ina kura moja sawa na China yenye watu bilioni 1.3 ambayo pia ina kura moja."

Maneno ya Zitto kwamba tusiingie mtego wa kujenga chuki yana maana kubwa sana na kwa kweli yanawajibu moja kwa moja viongozi wa Chadema bila kuacha hata chenga.

Yanawajibu viongozi wa Chadema ambao kauli zao ni kama vile haziwaheshimu Wazanzibari huku wakijaribu kupandikiza mbegu kwamba kwa kuwa Zanzibar ina watu wachache, hakuna sababu ya kuwapa idadi kubwa uwakilishi katika vyombo mbalimbali likiwemo Bunge.

Hivi karibuni, Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu alikaririwa katika mkutano wake mmoja akisema: "Huyu Rais (Samia) Mzanzibari, siyo Mtanganyika; kwa sababu ya miaka 60 ya Muungano, huyu Mzanzibari akatoka anakotoka kuja kuvuruga watu huku. Usingekuwa Muungano asingethubutu kwa sababu asingekuwa Rais."

Lissu pia alidai au kufafanua kwamba Samia anachovuruga huku Bara ni kile alichoita kuwafukuza Wamasai Ngorongoro na eti ameuza Bandari ya Dar es Salaam kwa Mwarabu kwa sababu yeye (Samia) si Mtanganyika.

Tangu akiwa Bungeni, Lissu alikuwa pia akihoji mara kwa mara ni kwa nini Wazanzibari ni wachache lakini wana uwakilishi mkubwa Bungeni.

Hata juzi, Lissu huyohuyo amehoji kwamba ni kwa nini Mbunge wa Zanzibar anawakilisha watu takribani elfu saba, lakini mbunge wa huku Tanzania bara anawakilisha wakati mwingine zaidi ya watu laki moja?

Watu wengi walilalaani kauli za Lissu wakiwemo baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wakisema ni za kebehi, chuki na kuidhihaki serikali na viongozi wake.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, Mwakilikishi wa mwavuli wa vyama 11 vya siasa, Juma Ali Khatib alisema Lissu hana nia njema kwa Watanzania kutokana na kuhubiri kauli za kibaguzi hasa kwa upande wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema Watanzania wana maadili yao, wakiongozwa na mila, silka na utamaduni katika misingi ya kuheshimiana na ndiyo sifa ya Mtanzania.

Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha ADA Tadea, alisema asili ya Tanzania linatokana na muunganiko wa wananchi wa pande mbili zilizokuwa huru pamoja na undugu wa damu wa mataifa mawili, hivyo siyo vyema kiongozi huyo kukebehi upande mmoja wa muungano huo.

Juma alimtaka Msajili wa Vyama vya Siasa nchini achukuwe hatua kwa mujibu wa sheria za vyama na vyombo vya ulinzi na usalama dhidi ya mwanasiasa huyo ili kuwa fundisho kwa watu wengine.

Alikumbusha kwamba lengo la Rais Samia Suluhu Hassan kufungua mikutano ya kisiasani ili viongozi wa vyama vya siasa kuendelea kunadi sera zao kwa kufanya mikutano ya kistaarabu, siyo kuzungumzia kauli za uchochezi, kejeli na ubaguzi

Naye Haji Ambari kutoka Chama cha NCCR-Mageuzi, alisema wakati huu Tanzania ikifikisha miaka 60 ya muungano siyo vyema kuzungumzia chuki za kuwagawa Watanzania bila ya sababu ya msingi au kwa uroho wa madaraka ya mtu fulani.

Alisema wakati umefika kwa Watanzania kutokukubali kugawanywa na wanasiasa ambao hawana nia njema kwa taifa lao hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuendelea kuhubiri umoja na ushikamano uliopo.

Lissu alipotoa meneno ya kibaguzi, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alizungumza bungeni akishangaa viongozi wa Chadema kutokemea maneno hayo ya ubaguzi ya Lissu na kukejeli urais wa Dk. Samia.

Kumbe imedhihirika kwamba la Lissu na la Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe ni moja. Katika katika mkutano wake wa hadhara wiki iliyopita, Mwenyekiti huyo wa Chadema, Mbowe, alidai kuwa Zanzibar wana Rais wao lakini wanatukopesha na sisi (Wabara) Rais wetu na kudai Bara (Tanganyika) tunatawaliwa na Rais wa nchi jirani kwa sababu visiwa hivyo ni nchi kamili!

Pia Mbowe alijifanya kushangaa inakuwaje Zanzibar yenye watu wasiozidi milioni moja na nusu wanatoa wabunge 80 kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mbowe akazidi kusema: "Tupo Watanzania milioni 64 leo, lakini tunatawaliwa na nchi jirani ya Zanzibar, yaani visiwa hivyo vinatukopesha sisi Watanganyika Rais. Zanzibar yote ina watu wasiozidi milioni moja na nusu halafu wanatoa wabunge 80 kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano; huu kama si uchizi ni nini?"

Haya maneno ukiyaangalia kwa ndani ni ya uchochezi lakini mimi sipendi kwenda huko.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipata kusema kwamba viongozi waliofilisika kisiasa hupenda kutumia dini na ukabila ili kuungwa mkono na ndicho kinachotokea kwa Chadema. Ni kama wamekosa cha kukosoa kwenye utendaji wa Rais Samia ndipo wamekuja na dhana ya Uzanzibari na Utanganyika.

Lakini pia Mwalimu Nyeerere alionya kwamba Zanzibar, hata tukiamua kwenda kwenye serikali moja, lazima isilinganishwe na Lindi kwenye uwakilishi. Yenyewe itakuwa na uwakilishi mkubwa.

Mwalimu alisema, "Watasema Wazanzibari hivi kweli mtawafanya kama watu wa Lindi? Wana watu laki saba (wakati huo). Lindi pia wana watu laki saba. Hivi kwa common sense, nchi zilizokuwa mbili... hata kama mtaafikiana kuwa na serikali moja. Nyinyi mnasema hivyo, Wazanzibari wanasema hivyo kwamba serikali mbili zinatuletea mgogoro, twende kwenye serikali mbili. Mka-move kwenda kwenye serikali moja, watu wenye busara watasema msiifanye Zanzibari kama Lindi. Watesema Zanzibari bado, representation (uwakilishi) yake katika Bunge haiwezi kuwa sawa na Lindi. Watu wenye nia njema watasema hiovyo.

"Ni kweli kuna watu watakuja kuuliza baadaye, mbona Zanzibari wana watu laki saba wana watu wengi katika Bunge hili kuliko Lindi. Maelezo yatakiwa ni historical (yataangalia suala la historia). Ndivyo ilivyo duniani siku zote. Hata watoto watakapokuwa wamesahau, lazima wakumbushwe kwamba Zanzibar huko nyuma, na Tanzania Bara, zilikuwa ni nchi mbili mbalimbali lakini yakawa mazungumzo tukaungana. Kwa hiyo hata kama mtakwenda kwenye serikali moja, kama nia ni njema, Zanzibar lazima itendewe tofauti na Lindi."



# ‘Dikteta’ Mbowe anavyomwonea wivu, husuda Rais Samia

Na Hamid Yassin

MACHI 25 mwaka huu, Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe akiwa kwenye mkutano wa hadhara wilayani Hai, Kata ya Bamang'ombe alidai kuwa, mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 alilazimika kukimbia nchi baada ya kunasa habari za kutaka kuuwawa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mwanasiasa huyo ambaye aliporudi nchini aliswekwa rumande hadi alipokuja ‘kuokolewa’ na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Alidail alikaa Kenya kwa miezi miwili kabla ya kukimbilia Dubai alipoweka maskani yake kwa muda mrefu kabla ya kurejea nchini.

“Nisingerudi, ningeendelea kukaa hukohuko lakini niliamua kurejea nchini baada ya kusikia wimbo wa ‘parapanda’ ukilia huku Tanzania,” Mbowe alieleza hadhara ile akimaanisha kwamba alirejea nchini baada ya kusikia taarifa kwamba Rais wa Awamu ya Tano, John Pombe Magufuli amefariki dunia.

Sitaki kurejea yote aliyosema Mbowe siku ile kwa sababu nilishaandika na wala si mada yangu ya leo, nimegusia tu nikitaka kuunganisha kauli ile kwamba alirejea nchini kwa kuwa, Rais wa nchi alikuwa ni mwingine ambaye ni Dk. Samia Suluhu Hassani!

Lakini nigusie tu kwamba katika mila zetu Waafrika ni mwiko kumsema vibaya marehemu na ni kosa au mwiko zaidi kumsingizia marehemu. Mababu waliozuia jambo hili bila shaka walijua watatokea akina Mbowe na kuwadingizia marehemu kila wanavyojisikia kwa sababu wanajua hayupo, hawezi kuwajibu.



### KUNGURU HAFUGIKI

Na kweli Dk. Samia alimsitiri sana Mbowe aliporejea nchini, kwani alidakwa na kuswekwa rumande ili akabiliane na kesi zake alizozikimbia wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano. Hii inaonesha dhahiri kwamba Mbowe alikuwa anakimbia kesi lakini anahadaa watu kwa kumsingizia marehemu.

Hata hivyo, Rais wetu kwa uungwana wake na kwa madaraka alio nayo kama kiongozi wa dola aliuomba mhimili wa mahakama umfutie kesi zake zote ili awe huru kufanya siasa.

Waswahili wana misemo yao kama vile; “Kunguru hafugiki,” “Binadamu hawana wema, ” na “Hasidi hana sababu!” Fadhila zote zile za Dk. Samia kwa Mbowe malipo yake ni haya ya kumbagua na kumwita ni Rais wa Tanganyika wa ‘kukopeshwa’ toka Zanzibar!

### KUFILISIKA KISIASA

Mbowe katika mkutano wake wa hadhara wiki iliyopita, alikwenda mbali na kudai, kuwa Zanzibar wana Rais wao lakini wanatukopesha na sisi (Wabara) Rais wetu na kudai Bara (Tanganyika) tunatawaliwa na Rais wa nchi jirani kwa sababu visiwa hivyo ni nchi kamili. Hivi



hawa wanapandikiza mbegu gani hii?!

Pia Mbowe alijifanya kushangaa eti inakuwaje Zanzibar yenye watu wasiozidi milioni moja na nusu wanatoa wabunge 80 kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mbowe si maamuma, ni msomi kwa kiasi chake na naamini anajua vizuri masharti ya kuungana kwa nchi hizi zilizokuwa huru kabla ya kuungana Aprili 26 mwaka 1964. Isipokua kwa makusudi anafanya mazingaombwe ya kisiasa!

“Tupo Watanzania milioni 64 leo, lakini tunatawaliwa na nchi jirani ya Zanzibar, yaani visiwa hivyo vinatukopesha sisi Watanganyika Rais. Zanzibar yote ina watu wasiozidi milioni moja na nusu halafu wanatoa Wabunge 80 kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano; huu kama si uchizi ni nini?” Alihoji Mwenyekiti huyo wa Chadema.

Huu ni zaidi ya uchochezi kwa kusigina katiba na kama ingekuwa enzi ya Serikali ya Awamu ya Kwanza ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere au ile ya Awamu ya Tano ya hayati John Pombe Magufuli; saa hizi Mbowe angekuwa mahabusu akisubiri kuburuzwaahakamani kufafanua kauli zake ambazo bahati ni nzuri ni wajinga tu wanaweza kumwelewa.

Angalau maneno haya yangekuwa yananenwa na Mwanademokrasia wa kweli, lakini yanatoka kinywani kwa dikteta namba moja wa kambi ya upinzani, ambaye hataki kuona wanasiasa wenzake wa kambi hiyo wakichanua kwenye medani za siasa za taifa hili.

Lakini sisi tuliosoma Cuba, tunajua kinachomtesa Mbowe na wenzake ni kukosa hoja kutokana Rais Samia kutoshikika kila mahala kwa kuupiga mwingi. Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alipata kusema kwamba mwanasiasa anafilisika kisiasa, mara moja hutafuta kuungwa mkono kwa kutumia dini au ukabila (umajimbo). Watanganyika wana shida gani na Uzanzibari wa Rais Samia kama anaowaongoza vizuri?

### MTAFURUKU NDANI YA CHADEMA

Waswahili wanasema lisemwalo lipo kama halipo laja. Hivi sasa umezuka mtafaruku mkubwa ndani ya Chadema, kisa ni uchaguzi wa ndani wa chama hiki ambapo Mbowe





ameingia kwenye malumbano makubwa na Makamu wake, Tundu Antiphas Lissu akihisi jamaa anaitaka nafasi yake ya Uenyekiti!

Na kimsingi, wote wawili hawafai kwa sababu nyingi moja wapo ni wote kuwa na vinasaba vya udikteta na kukosa busara za kiuongozi. Lakini kwa nini wote hawafai kama Chadema inataka kutoka iliko na kuwa chama kitakacholeta upinzani mkali kwa CCM ni mada nyingine nitakayoitayarisha siku nyingine.

Sasa hivi Chadema imegawanyika katika makundi mawili, 'Timu Mbowe' na 'Timu Lissu' kiasi cha kuvuruga hata chaguzi zao za Kanda! Mbowe anawataka kina Godbless Lema, Joseph Mbilinyi 'Sugu' na wengine wanaomtii waongoze Kanda zao za Kimajimbo, lakini Lissu naye ana watu wake anaowapigia kampeni washike nafasi hizo akina Peter Simon Msigwa!

Lissu anasema kuna fedha chafu na ufisadi mkubwa katika uchaguzi wa ndani wa chama hiki mwaka huu na anahoji fedha hizi za kukivuruga chama chao kambi ya Mbowe wamezitoa wapi?

Kwa madudu haya ndani ya Chadema Mbowe anatoa wapi nguvu za kuhoji uhalali wa Urais wa Dk. Samia ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Wahenga wanasema kabla ya kutoa kibanzi kwenye jicho la mwenzako angalia kwanza boriti iliyopo kwenye jicho lako!

### USHAURI WA BABA WA TAIFA

Mbowe amefanya mambo mengi ya ajabu ndani ya chama chake, ametengeneza maadui wengi ndani na nje ya Chadema; hivyo kila anayemwona mbele yake anahisi ni adui yake, hebu ageuke nyuma amwone adui yake halisi. Ni hichohicho kivuli chake, hakuna kingine!

Wakati inaanzishwa Chadema nakumbuka Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alimtaka mwasisi wake, Mzee Edwin Mtei kuzingatia demokrasia ya kweli na si ya kupakana mafuta kwa mgongo wa chupa.

Mwalimu akamtakia heri na kumtaka alielewe vyema neno "Demokrasia" kuwa demokrasia si umangimeza, bali ni urari wa siasa, uvumilivu na kukubali kushindwa.

Aidha, akamwambia kuwa demokrasia hailei vurugu, uzandiki, wala kinyongo. Kwamba demokrasia inamwekea ukomo kiongozi wake hata awe mwasisi. Kikubwa kuliko vyote ni kwamba demokrasia hutaka watu wapokezane vijiti kwa utaratibu mahsusi.

Lakini wosia huo wa Baba wa Taifa kwa Mzee Mtei umekuwa sawa na kaa la moto. Kwani Chama hicho kimekuwa kana kwamba ni cha kiukoo.

Kwa nini nasema hivi? Ndiyo; nasema hivi kwa sababu Mzee Mtei alipostaafu Uenyekiti wa Chadema alimkabidhi wadhifa huo, Mzee Bob Makani ambaye walikuwa na 'ushemeji' baina yao.

Baada ya kuondoka kwa Makani (sasa ni marehemu), Mzee Mtei akamkabidhi mkwewe Uenyekiti wa Chama hicho. Mkwewe huyu ni nani? Ndiye huyu Freeman Aikaeli Mbowe ambaye mpaka hivi ninavyoandika makala haya amekalia kiti hicho kwa zaidi ya miaka 20 hadi sasa na hakuna dalili zozote zinazoonesha atakiachia labda kwa kung'olewa au vurugu na mapambano.

### KITI CHA MBOWE MOTO!

Nathubutu kusema hapa kuwa kila aliyethubutu kuwania nafasi hii ya Mbowe alifanyiwa mizengwe mpaka akafukuzwa uanachama. Kama mimi muongo, basi waulizeni Zitto Zuberi Kabwe, Samson Mwigamba na Kitila Mkumbo.

Kana kwamba hiyo haitoshi, kuna sakata la marehemu Chacha Zakayo Wangwe ambalo mpaka leo hii miaka 16 baada ya kufa halijapatiwa suluhu wala ufafanuzi wa tija kuhusu jinsi alivyokufa kwenye ajali ya utata ya Julai 27 mwaka 2008 kule Dodoma akiwa Makamu Mwenyekiti wa Chadema.

Mbowe ni mtu ambaye watu walimsema vibaya kuhusu kifo cha Wangwe ambaye alipoutaka uwenyekiti wake wakavurugana vibaya.

Mwaka 2021, mjane wa Chacha Wangwe kwa wanaokumbuka, Mjane wa Chacha Wangwe, Ghati Wangwe akiomba serikali ifanya uchunguzi wa kifo cha mumewe.

Wengine ambao walishindwa kukielewa vyema Chama hicho kuwa si cha kidemokrasia kama kinavyojiita ni kaka yangu John Shibuda na Said Arfi aliyekuwa pia Makamu Mwenyekiti wa Chadema kabla naye kujiuzulu ghafla Novemba 22 mwaka 2013! Hawa wawili walijiunga na chama hicho kwa mbwembwe na vishindo kwa kutegemea kuwa kiko sawa na jina lake.

Masikini hawakujua kabisa kuwa chama hicho ni cha wanaharakati na kina wenyewe kina-Mtei na wafuasi wake.

Kana kwamba hiyo haitoshi, watu wamuulize Dk. Wilbrod Slaa kilichomkuta. Bila ajizi wala majungu, Dk. Slaa alifanya kazi kubwa mno ya kukikuza chama hicho na kukifanya kuwa imara alipojiunga nacho akitokea CCM.

Lakini leo hii yuko wapi? Kabakia kuwa kibaraka wa kujikomba kwenye mikutano ya hadhara na maandamano yao baada ya CCM na Serikali yake kuchoka kumstiri tangu alipojitengea na Chadema mwaka 2015.

Niseme wazi hapa kwamba Mbowe lazima ajifunze demokrasia kwa wapinzani wenzake ambao si wengine bali ni Hamad Rashid Mohammed na Zitto Zubeir Kabwe.

Hamad Rashid Mohammed aliwataka viongozi wa vyama vya siasa nchini kuweka ukomo wa uongozi.

Alisema yeye, iwapo Mwenyezi Mungu (SW) atamjaalia ataongoza chama hicho kwa miaka kumi tu na baada ya hapo atawaachia wengine.

Alisema ni vyema kabisa kwa vyama vya siasa kuwa na utaratibu wa kuwatayarisha watu kuwa viongozi badala ya viongozi waliopo kuwa madarakani bila kikomo.

Kwamba uongozi bora ni ule wenye ukomo na siyo ule wa milele mpaka mtu afe. Kwani uongozi wa aina hiyo ni waziwazi kuwa ni usultani kama siyo ufalme.

Sultan au Mfalme anapokufa lazima arithiwe na kaka yake, mtoto wake au nduguye yeyote. Wenyewe wanasema eti damu isitoke nje! Lo! Usultani hadi ndani ya chama cha siasa, hatari kubwa!

Hamad Rashid aling'atuka Chama cha Wananchi (CUF) akiwa ni kiongozi wa nafasi za juu, alianzisha rasmi na Chama cha Alliance For Democratic Change (ADC), ambacho ametanabahisha kwamba hataki kukaa milele kwenye uongozi kabla ya kuwachia wengine.

Ni kwa mtaji huo basi, wakati umefika wa Mbowe kuachia nafasi yake kwa wengine. Aache kabisa umangimeza kwani tabia hiyo itaua Chadema.

Nasema hivi kwa sababu endapo watu hawatakuwa wakitayarishwa ndani ya vyama vyao, kutakuja tokea balaa kubwa la kutokuwa na viongozi waadilifu.

Badala yake tutakuja kuwa na madikteta ambao kwao uongozi ni vita, malumbano, mapigano na kelele zisizokuwa na tija kama hizo zinazotekelezwa na kina Mbowe, Tundu Lissu na wafuasi wao.

Tanzania inahitaji viongozi wenye tija. Viongozi ambao watakaelewa kuwa vyama vya siasa si NGO's za watu bali ni vya wanachama wao na kwamba yeyote anaweza kukalia kiti iwapo atachaguliwa na kuaminiwa.

### UDIKTETA WA DHAHIRI

Utafiti unaonesha wazi kuwa wale wote wanaong'ang'ania uongozi kwenye vyama huwa madikteta wanapoingia Ikulu na kwamba huwa hawako tayari kung'atuka kama alivyofanya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1985 alipomwachia nchi Mzee Ruksa, hayati Ali Hassan Mwinyi!

Mwalimu Nyerere aling'atuka kwenye uongozi wa Serikali mwaka 1985 na baadaye akang'atuka kwenye uongozi wa Chama chake mwaka 1987.

Alipokuwa akiachia Uenyekiti CCM, Mwalimu alisema wakati umefika wa kuamini watu wengine kushika wadhifa mkubwa kama huo ili kuifanya nchi iwe tulivu na yenye amani.

Zitto Kabwe ameweza pale ACT Wazalendo akiwa bado kijana mdogo mwenye nguvu, Mbowe unashindwa nini kufanya hivyo hapo Chadema? Shauri yako endelea kumwonea wivu Dk. Samia na Wabunge wa Zanzibar kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano huku wewe mwenyewe unajichimbia 'kaburi' ndani ya Chadema. Sijui utamweleza nini Mzee Mtei kina Lissu wakishika hatamu ya chama chenu!

***Kwa ushauri na maoni; 0768 888 787 au 0784 122 020.***



# Je, vyakula vya kuongeza heshima ya ndoa vinafanya kazi kweli?

**Mwandishi Wetu na mashirika ya Kimataifa**

DOKTA Cuthbert Maendaenda ambaye alikuwa meneja wa Mradi wa Ushiriki Sawa wa Wanaume katika Haki ya Afya ya Uzazi na Ujinsia (TMEP) mradi ambao haupo kwa sasa, wakati fulani akizungumza kwenye semina na waandishi wa habari alisema kile ambacho kimekuwa kikisababisha baadhi ya wanaume kushindwa kuwatosheleza wenza wao kunako sita kwa sita, asilimia zaidi ya 60 ni sababu za kisaikolojia.

"Mwanaume ukiwa na hofu kwamba leo pengine nitashindwa ku-perform, kweli utashindwa. Lakini mwenza akiwa mchafu au kugundua maumbile ambayo hukutarajia pia kama ndio unakutana naye kwa mara ya kwanza, inaweza kusababisha ukashindwa ku-perform. Na hii ni kwa jinsia zote mbili," alisema Maendaenda.

Lakini alisema sababu nyingine inayowafanya wanaume kushindwa kuleta heshima ya ndoa nyumba ni magonjwa ikiwemo kisukari.

Alisema sababu nyingine ni vyakula. Kwamba kutotumia vyakula bora inaweza pia kusababisha mwanaume ashindwe ku-perform sawasawa pale anapojifungia na mwenza wake kwenye kuta nne. Kwamba vyakula duni pia vinaweza kupunguza hamu ya mwenza mwenye jinsi ya 'ke' kuhitaji 'chakula cha usiku'.

Kwa mujibu wa daktari huyo, baadhi ya watu wanaamini kwamba kuna vyakula vinavyofanana na mbegu za kiume kama karanga, nazi au mihogo kwamba vinasaidia kuongeza nguvu za kiume. Anasema vinaweza kusaidia kutegemea virutubisho vilivyomo lakini si kwa sababu ya kufanana huko.

"Ni kama kuna matunda mekundu yanaitwa matunda damu. Watu wanadhani kwa sababu yanafanana na damu ukiyala basi unapata damu moja kwa moja. Si sahihi. Ukila haya matunda yataingia kwenye mfumo wa chakula na mwili utanyonya virutubisho vililivyomo na unaweza kukuta hakuna hata madini ya chuma yanayosaidia katika utengenezaji wa damu.

"Vivyo kwa vitu kama karanga au supu ya pweza. Ukila vitaingia mwilini kama vyakula vingine. Cha masingi ni mwanaume kula mlo wenye virutubusho vyote muhimu na kwa wakazi wa mijini wanaofanya kazi kubweteka na kutumia sana magari kuhakikisha wanafanya mazoezi," anasema.

Katika andiko moja kwenye mtandao wa BBC, masuala la vyakula na suala zima la wanaume kuleta heshima ya ndoa nyumbani limezungumziwa pia.

Chokoleti, stroberi, chaza andiko alinsema vyakula ambayo huelezwa kwamba vinaweza kuongeza hamu ya watu kukurubiana na wenza wao. Je, kuna ukweli wowote kwenye madai hayo?

Kwa mujibu wa andiko hilo, wale ambao wana matatizo kwenye performance yao ni kweli vyakula fulani vinaweza kusaidia kwa njia moja ama nyingine.

Andiko linasema jamii mbalimbali katika historia zimekuwa zikitumia vyakula ambavyo vinaweza kuongeza hamu ya ku-perform.

"Hata hivyo, watu walio na matatizo katika ufanyaji wao wa mapenzi ndio huona mabadiliko wanapokula hivi vyakula," anasema Lauri Wright, msemaji wa Chuo cha Nutrition and Dietetics cha Marekani. "Mtu asiye na matatizo hawezi kuona mabadiliko yoyote."

Chakula kimoja ambacho kinaaminika kwa muda mrefu kuongeza nguvu za kiume ni chokoleti. Utafiti unaonyesha kuwa kakao pia ni zao ambazo linaweza kuongeza hamu ya ku-perform.

Kula chokoleti kunaweza kuongeza hamu ya kufanya 'mambo yetu yale' kwa kuchochea utengenezaji serotonini na kemikali ya dopamini ya nyurotransmita, ambazo pia huchangia katika mwitikio wetu wa katika ku-perform.

Michael Krychman, mtaalamu na mshauri wa masuala ya kujamiiana kutoka kliniki ya Sexual Health and Survivorship Medicine, Marekani anasema "tunachojua ni kwamba, watu wanaofanya mazoezi, kula lishe bora na kupunguza msongo wa mawazo, vitu hivi vyote huboresha maisha ya wanapokuwa wanataka ku-perform."

"Mlo wetu unaweza kufanya kazi kama kichochezi kutupa manufaa kama vile mtiririko mzuri wa damu, kuongezeka homoni au kuongeza hamu ya ku-perform," anasema Wright.

"Jambo la msingi kuzingatia ni kula samaki, kula nyama isiyo na mafuta, karanga, matunda, mbogamboga na nafaka. Hivi huasaidia kazi ya neva na kusaidia mtiririko wa damu na homoni," anasema Wright.

"Hamu ku-perform pia ni suala la kisaikolojia. Ukweli ni kwamba hamu ya kushiriki na mwenza ina mambo mengi. Dawa au chakula vinaweza kufanya kazi," anasema Nan Wise, mtaalamu wa saikolojia na masuala ya kujamiina katika Chuo Kikuu cha Rutgers cha New Jersey, Marekani.

"Uzoefu wetu pia unaweza kuchangia kujua ni vyakula gani vinavyoongeza hamu ya kutaka ku-perform kwa mtu mmoja mmoja," anasema Jean-Christophe Billeter, profesa wa tabia za kijamii na kujamiiana katika Chuo Kikuu cha Groningen nchini Uholanzi.

"Ubongo unakuwa na waya wa kutengeneza kumbukumbu tunapopata mafanikio ya tendo la ndoa, kulingana na hali itakavyotokea katika mazingira ambayo mtu ali-perform, hii itakuwa ni kitu cha kuamsha hamu ya kukutana na mwenza."

Kuna utafiti unapendekeza kuwa mawazo chanya yanahusishwa na kuongezeka kwa msisimko wa mwili kuhitaji ku-perform, na mtu kupata lishe iliyo na vyakula vingi vinavyotokena na mimea.

Inawezekana chakula chochote kinaweza kuwa na sifa za kuongeza hamu ya ku-perform. Kwa maana kwamba, ikiwa mtu ana njaa na hakuna chakula, hamu yake ya kukutana na mwenza kunako sita kwa sita itapungua.

Kimsingi, wanadamu, mke na mume hukutana wakiwa wamejifungua chumbani ili kuzaliana, na tunahitaji kuwa na uzito mzuri na kuwa na lishe ambayo hutoa virutubisho sahihi ili kufanya hivyo, anasema Billeter.

Pia kuna ushahidi kwamba tunakula vyakula vinavyotufanya tuonekane tunavutia kwa watu wa jinsia tofauti. Fikiria ndege fulani, madume wana rangi nyingi zaidi kwa sababu majike wanavutiwa nazo, na wanapata rangi hii kwa kula vyakula fulani.

Hiyo ipo kwa wanadamu pia. Hapo awali, wanawake walionekana kuwa na mvuto zaidi kwa wanaume wanapokuwa wanene lakini sasa mtazamo umebadilika," anasema Bileter.

"Buibui hukamata nzi ili kumwasilisha kwa majike ili kujamiiana nayo, wakati nyenje huzalisha jeli ili kuwashawishi majike kujamiiana nao," anasema Abbott.

# Kutana na binadamu mwenye figo nne mwilini mwake



WENGI wanafahamu kuwa kwa kawaida, binadamu ana figo mbili katika mwili wake, lakini hivi karibuni nchini Somalia, aligundulika mtu mmoja akiwa na figo nne.

Kuna watu watatu pekee wenye figo za ziada zilizorekodiwa duniani kote na mtu wa nne sasa amepatikana nchini Somalia.

Watu wenye figo za ziada, huwa hawajitambui mpaka pale wanapopatwa na hali ya kiafya inayowalazimu kumtembelea daktari, bila kujua juu ya ukuu wa ziada ambao Mungu amewapa, lakini hugundua tu wanapopima, na wanafahamu baada ya uchunguzi wa ultrasound au baada ya upasuaji.

Mvulana mdogo ambaye madaktari hawakumtaja jina lake, aliugua na baada ya uchunguzi wa muda mrefu, aligundilika a kuwa ana figo nne.

Hospitali ya Mafunzo na Utafiti ya Kituruki nchini Somalia, iliyokuwa ikijulikana kwa jina la Digfeer, ilitembelewa na mgonjwa huyo aliyekuwa akilalamikia maumivu kwenye figo yake ya kushoto.

Baada ya madaktari kumfanyia uchunguzi, walibaini kuwa mgonjwa huyo ana figo nne.

Dk. Abdikarin Hussein Mohamed Gabayre, daktari wa mfumo wa mkojo na upasuaji wa uzazi wa kiume ambaye alimfanyia mgonjwa upasuaji, aliambia BBC jinsi walivyofahamu hali hiyo.

"Mgonjwa aliyetembelea hospitali aligundulika kuwa na hali hii baada ya kufanyiwa uchunguzi, ilishangaza kwa sababu watu watatu tu ndio walikuwa wanajulikana duniani na atakuwa mtu wa nne, baada ya hapo tukatafuta njia bora ya matibabu ya mgonjwa huyu kwani ni tofauti na watu wengine".

Mgonjwa huyo pia alifanyiwa upasuaji kutokana na maumivu aliyokuwa akiyalalamikia kutokana na jiwe lililokuwa kwenye fupanyonga lake la kushoto.

### JE; KUNA FAIDA NA HASARA YA KUWA NA FIGO NNE?

Mgonjwa huyo alikuwa akisumbuliwa na mawe kwenye figo kwa muda na madaktari walisema kuwa kunywa maji machafu na kula nyama nyekundu, pamoja na mambo mengi, ni chanzo cha mawe kwenye figo.

Kwa mgonjwa huyu mwenye figo nne, figo zake ziko na afya nzuri na zinafanya kazi kwa kawaida, ni dhahiri kwamba figo mbili za upande wa kulia hazitegemei kila mmoja, wakati figo mbili za upande wa kushoto zimeunganishwa kwa sehemu.

Figo ambayo mara nyingi huwa inakabiliana na pombe na bidhaa taka, huwa inakabiliwa na ukuaji wa mawe, jambo ambalo madaktari walieleza kuwa ndio sababu mgonjwa huyu anaathirika zaidi na mawe kuliko watu wa kawaida ambao wana figo mbili.

"Siyo athari au tatizo maalum mgonjwa huyu kuwa na figo nne, bali ni rahisi kupata matatizo ya figo yanayohusiana na mawe, kwa kuwa ana figo nne, anaweza kuhisi maumivu kama watu wa kawaida wana figo mbili lakini maumivu yake ni zaidi ya kawaida," alisema Dk Gabayre.

### JE WALIO NA FIGO NNE NI BORA KULIKO WALIO NA MBILI?

Madaktari wanasema kwamba ubora wa figo zake nne ni sawa na mtu mwenye figo mbili na hakuna faida zaidi ya watu wa kawaida, kama ni kwa utendaji na kazi.

Inafaa pia kuzingatia kwamba ikiwa figo zake mbili zitatolewa, ni sawa na mtu aliye na figo mbili, ambayo inamaanisha kuwa ana upungufu.

Madaktari hao waliishauri familia ya mgonjwa kufuatilia na kuchukua uangalizi maalum, na pia walisema kila inapohitajika matibabu anahitaji huduma tofauti na ilivyozoeleka kwa kuwa hali yake ni tofauti na watu wengine. *BBC.*



Dk. Abdikarin Hussein Mohamed Gabayre



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Kongole Samia uwekezaji huu mkubwa madaktari bingwa

Mwanafalsafa mmoja wa kiroho aliwahi kusema kwamba mtu aliyepewa dunia na muumba wake ni yule anayeamka asubuhi akiwa na vitu vitatu vifuatavyo: amani, chakula cha siku hiyo na afya.

Kuhusu suala la afya ambalo makala hii linaiangazia zaidi, utoaji wa huduma bora kwa wagonjwa unategemea uwepo wa vitu vingi, lakini kubwa miongoni mwa hayo ni uwepo wa wataalamu wenye ujuzi, maarifa na weledi.

Kukosekana kwa wataalamu wa kuwahudumia wagonjwa, kunapelekea vifo na matumizi makubwa ya fedha kwani wagonjwa watalazimika kwenda nje ya nchi kutafuta matibabu, jambo linaloongeza gharama za matibabu kutokana na kugharamia nauli, chakula, malazi na matibabu yenyewe.

Na kumbuka hilo la kwenda nje kutafuta matibabu wanaomudu ni wachache na hivyo naweza kusema tumepoteza Watanzania wengi miaka ya nyuma kutokana na kukosa madaktari bingwa na bobezi katika nchi yetu. Gharama za kutibiwa nje mara nyingi huwa zaidi ya mara mbili kama ugonjwa uleule utatibiwa hapa nchini.

Ni ukweli uliodhahiri kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi shupavu wa Dk. Samia Suluhu Hassan umejipambanua pasi na shaka kuipa msukumo na kipaumbele sekta ya afya kwa kuboresha miundombinu, upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, na kuwajengea uwezo raslimali watu ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) inatoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaosomea kozi mbalimbali, ambapo miongoni mwa hizo ni wanafunzi wanaosoma kozi za afya ili kuongeza wigo wa wataalamu wa afya watakaotumia maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali katika kuwahudumia Watanzania.

Katika eneo ambalo bado hatujawa na wataalamu wa kutosha ni la ubingwa na ubingwa bobezi. Kutokana na uhaba wa wataalamu hawa, Rais Samia ameweka mkakati wa kutoa ufadhili wa masomo unaogharimu bilioni 10.9 ili Watanzania wengi waweze kusoma na hatimaye kupunguza upungufu uliopo sasa katika eneo hilo muhimu.

Fedha hizi zimetengwa ili kuwezesha wanafunzi 1,109 kwenye masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi kupitia mradi wa Dk. Samia Super-Specialized Scholarship Programme kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Akifungua Mkutano wa Mwaka wa Chama Cha Madaktari Bingwa na Magonjwa ya Ndani Tanzania (APHYTA) jijini Dar es Salaam, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alisema: "Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa madaktari bingwa katika kuwaendeleza kitaaluma kupitia programu ambayo imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa kwa mwaka wa masomo 2023/2024, kwa wanafunzi 1,109 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 582 ukilinganisha na mwaka wa masomo 2022/2023."

Utoaji wa ufadhili wa masomo kwa madaktari bingwa na bingwa bobezi ni njia bora inayohakikisha upatikanaji wa wataalamu wa uhakika kwa manufaa ya nchi yetu badala ya kutegemea wataalamu kutoka nje ya nchi kuja kutoa huduma nchini kwetu ambao wanagharimu fedha nyingi kuwaleta nchini au kupeleka wagonjwa wetu nje.

Ni jambo muhimu kwa taifa kujitosheleza kwa wataalamu wake wa ndani ili kuwa na uhakika wa huduma bora za afya.

Hivyo basi, uwekezaji huu mkubwa wenye lengo la kuhakikisha nchi yetu inakuwa na madaktari bingwa na bingwa bobezi ni jambo la kupongezwa sana.



Madaktari hawa wanategemewa kutoa huduma ya matibabu ya magonjwa ya akina mama na uzazi, magonjwa ya ndani kama vile shinikizo la damu, kisukari, figo, magonjwa ya watoto, mifupa, upasuaji, upasuaji wa meno, pua na koo, upasuaji wa watoto wenye midomo sungura, masikio, ngozi, moyo, mfumo wa chakula pamoja na magonjwa ya saratani.

Wataalamu hawa watakapohitimu masomo yao, watakuwa na jukumu la kutumia elimu waliyoipata katika kuwahudumia wananchi wa maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Huduma watakazozitoa kwa wagonjwa zitasaidia sana kuokoa maisha ya wananchi kwani kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa na upungufu wa wataalamu hawa ambao ni muhimu sana kwa mustakabali wa afya na ustawi wa wananchi.

Kutokana na maboresha makubwa katika sekta ya afya, wapo wagonjwa kutoka nchi mbalimbali za Afrika ambao sasa wanafuata huduma za afya Tanzania. Kwa hiyo, uwepo wa madaktari hawa bingwa na bingwa bobezi sambamba na serikali ya Dk. Samia kuleta vifaa tiba za kisasa, kunatoa fursa kwa sekta ya afya kuongeza mapato kutokana na kupokea wagonjwa wa ndani na nje ya nchi wanaofuata huduma za afya Tanzania na hivyo kunyanyua utalii wa kimatibabu nchini mwetu.

Akizungumza wakati wageni kutoka Sierra Leone walipowasili katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge alisema: "Tumepata ugeni wa wenzetu kutoka Sierra Leone wamekuja kuona maendeleo haya kuanzia tulipoanza hadi sasa wamekuja kujifunza viongozi wetu wanavyotuongoza na kuwa na taasisi kama hii. Vilevile wamekuja kuona utendajikazi wa wahudumu wetu wa afya wanavyofanya kazi ili wanapokwenda kuanzisha taasisi kwao wawe na uelewa wa kutosha.

"Pili wamekuja kujifunza ili kuleta wagonjwa kutoka Sierra Leone kuja kutibiwa hapa kwani wamejionea wenyewe kuwa watatibiwa vizuri na hii ni sehemu ya tiba utalii ambayo Rais pia amefanya."

Ni jambo la faraja kuona Tanzania leo imekuwa shamba darasa katika sekta ya afya kwa mataifa mengine kuja kujifunza na kutibiwa. Haya yote yanatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema.

Katika muktadha huo, Waziri Ummy alisisitiza: "Kupitia muundo huu mpya wa Sekta ya Afya, tutaweza kuwatambua kwa kuwawekea mazingira mazuri madaktari wenye ubobezi katika maeneo mbalimbali ikiwemo wa masuala ya magonjwa ya ndani."

Kuwatambua na kuwawekea mazingira bora madaktari bingwa na bingwa bobezi ili kutoa huduma kwa wananchi ni muhimu sana kwani itawavutia kufanya kazi ndani ya nchi na katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na hivyo kuwafikia wananchi wengi kwa huduma bora za kimataifa.

Vipaumbele sita vya kisera vya sekta ya afya kwa mwaka 2024/2025 ni pamoja na raslimali watu. Raslimali watu ni wataalamu wa afya ambao wizara imepanga kuwajengea uwezo kwa kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuendana na mazingira na mahitaji ya utoaji wa huduma bora za kiafya za kisasa na zenye viwango bora.

Ikumbukwe kuwa dhamira ya Rais Samia ni kupata wataalamu bingwa na bobezi wa kutosha wa kuweza kuhudumia halmashauri zote 184 hapa nchini na ndiyo maana kila mwaka kumekuwa na ongezeko la raslimali fedha zinazotengwa kwa ajili ya kufanikisha azma hii.

Mathalani kwa mwaka wa fedha 2021/2022, serikali ilitenga bilioni 3, mwaka 2022/2023 bilioni 8 na mwaka 2023/2024 bilioni 10.9 ili kusomesha madaktari bingwa na bingwa bobezi katika magonjwa mbalimbali.

Mei 6, 2024 Waziri Ummy Mwalimu alizindua Mpango Kabambe wa Madaktari Bingwa wa Rais Samia Katika Hospitali za Wilaya. Uzinduzi huu ulifanyika kwenye Hospitali ya Manispaa ya Iringa (Frelimo), Iringa, huku ukichagizwa na kaulimbiu isemayo "Tumekufikia, Karibu Tukuhudumie."

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, miongoni mwa mafanikio ya wataalamu hawa ni kupunguza vifo vya watoto wachanga. "Mpango Kabambe wa Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia utasaidia kupunguza vifo vya watoto wachanga kwa kuwajengea uwezo watoa watoa huduma wengine katika hospitali za halmashauri kwa kuwa dhamira ya serikali ni kuwa na wodi maalumu za watoto wachanga (NCU) katika hospitali hizo kuokoa maisha ya watoto wachanga wenye siku 0-28.

Tunaweza kuokoa maisha ya watoto wachanga endapo tutaanzisha wodi maalumu za watoto wachanga, tukaviwekea vifaa tiba ili endapo mtoto akiwa na changamoto yoyote aweze kupata huduma," amesisitiza Waziri Ummy.

Vilevile, kwa mujibu wa Waziri Ummy, Rais Samia ameweka rekodi duniani kwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 80, kutoka vifo 556 kati ya vizazi hai 100,000 kwa mwaka hadi vifo 104 kati ya 100,000.

Wakati serikali ikiendelea kusomesha watalaamu hawa ili kuongeza idadi kubwa zaidi, madaktari bingwa na bobezi waliopo sasa wanawajengea uwezo madaktari wengine katika halamshauri mbalimbali nchini huku wakitoa huduma za kibingwa kwa wananchi.

Dhamira ya Rais Samia ya kuhakikisha huduma bora za kibingwa zinatolewa nchini na kuwafikia wananchi wote ili kupunguza gharama za kutibiwa nje ya nchi haina tone la shaka. Kwani nikisema Mama Samia hana baya kwenye sektya ya afya, nitakuwa nimekosea kwa uwekezaji na utashi mkubwa wa kisiasa aliouonyesha katika kipindi kifupi cha uongozi wake?

Kongole Mama Samia kwa kuipa msukumo mkubwa sekta ya afya nchini kwa maendeleo na ustawi wa maisha ya wananchi. Watanzania sasa tunaamka tukiwa na uhakika pia wa afya zetu mbali na amani pamoja na chakula. Hayo mawili; chakula na amani jinsi Rais Samia anavyoyapambania kupitia mikati yake na R zake nne, nitayajidili siku nyingine panapo majaaliwa.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*

# Siku 1,000 tu zinaweza kujenga maisha mwanao au kuyaharibu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ninajiandaa kuandika makala haya, niliongea na mama mmoja mjamzito, mkazi wa Temeke, Dar es Salaam, Lucy (sio jina lake halisi), na kumuuliza kuhusu chakula anachopata kila siku kwa ajili yake na mtoto aliyeko tumboni.

Mama huyo ambaye huu utakuwa uzazi wake wa tatu kama atajaaliwa kujifungua salama aliniambia kwamba, kwa kawaida asubuhi hunywa chai ya rangi na muhogo.

"Mimi ninapendelea sana muhogo wa kuchemsha au wa kukaanga ingawa mara nyingine ninasukumia kwa chapati, maandazi au vitumbua," anasema Lucy.

Mama huyo anaendelea kueleza kwamba mchana kwa kawaida hula ugali wake wa sembe kwa nyama au samaki, ingawa anasema wakati mwingine samaki humpa hali ya kichefuchefu.

"Niliwahi kuambiwa kwamba kwa hali yangu (ya ujauzito) kula samaki ni muhimu, kwa hiyo huwa nalazimishalazimisha kula," anasema.

Kuhusu mlo wake wa usiku, Lucy ananiambia kwamba mara nyingi hula wali kwa maharagwe, au samaki na kwamba mara moja moja akiwa na fedha ananunua chipsi kwa kuku (wa kisasa) au mayai (ya kuku wa kisasa) na 'kusukumizia' kwa soda baridi.

Nilimuuliza mama huyu kama katika mlo wake wa kila siku anahakikisha unakuwa na mboga za majani au tunda, akajibu kwamba siyo kitu anachozingatia sana.

"Kuna wakati nikiwa na hamu ya mlenda, kisamvu au matembele ndio ninanunua. Mimi napenda sana kisamvu na mlenda hivyo angalau kwa wiki ninakula kimoja wapo," anasema.

Kuhusu matunda, mama huyo anasema si mpenzi sana wa matunda lakini anasema huwa anakula mara moja pale mume wake anaponunua lakini yeye si rahisi kutoa pesa yake kununua tunda!

Nilimuuliza Lucy kama anajua lishe ni nini? Akajibu kwamba anachofahamu yeye lishe ni ule unga maalumu uliochanganywa mahindi, mtama, ulezi na unga wa soya.

Swali la msingi nililokuwa ninatafuta kwake na ambalo ndilo limebeba maudhui ya makala haya, nilitaka kufahamu kama anajua lolote kuhusu umuhimu wa siku 1,000 za mtoto.

Nilitegemea ajibu kwamba hajui, lakini ninashukuru kwamba Lucy aliwahi kusikia umuhimu wa siku hizo alipokuwa na mimba ya mtoto wake wa pili. Nilipomuuliza anifafanulie maana ya siku hizo elfu moja kwa mtoto, hapo ndipo ilikuwa 'lugha gongana'.

"Nakumbuka walisema hizo ni siku ambazo mzazi unapaswa kuwa karibu na mtoto na kuhakikisha anakula na kushiba," alijibu.

Lucy, pengine anawakilisha idadi ya wazazi wengi wakiwemo akina baba. Kwa kuwa hivi karibuni nilishiriki kwenye semina inayohusu masuala ya lishe iliyotayarishwa na Jukwaa la Lishe Tanzania (PANITA) nilichukua fursa ya kumfafanulia Lucy haya yafuatayo.

Ni kwa ufafanuzi huu, tutaangalia kama mama huyu mjamzito anakula lishe bora na kama kuna madhara yoyote kwa mwanae aliyeko tumboni.

### SIKU 1,000 NI ZIPI?

Kwa mujibu wa Mratibu wa Programu wa PANITA, Jane Msagati, Siku 1,000 huhesabiwa toka mimba inapotungwa mpaka pale mtoto anapotimiza umri wa miaka miwili, yaani anapofanya sherehe yake ya pili ya kuzaliwa.

Jane anasema siku hizi ni muhimu sana kwa kuwa ndio msingi wa maisha ya binadamu yeyote.

Anasema wazazi ni muhimu kuzingatia lishe bora katika siku hizo1,000 kwa kuwa matokeo yake huendelea kwa kipindi chote cha maisha ya mwanadamu na kwamba mtoto akishaathirika katika siku hizi kutokana na upungufu wa lishe huwezi tena kurekebisha upungufu huo.

Umuhimu wa siku 1000

Jane Msagati anasema lishe bora kwa siku 1,000 huokoa vifo vya watoto zaidi ya 1,000,000 kwa mwaka duniani na kwamba kama zitatumika vizuri huongeza kiwango cha kuelewa cha mtoto na kumwezesha kufanya vizuri shuleni na maishani kwa ujumla. Hii inatokana na ukweli kwamba mtoto akikosa lishe bora katika hizo siku 1,000 mara nyingi hupata udumavu ambao ni hali ya ubongo wake kutokua katika kiwango kinachotakiwa.

Kiuchumi, kwa mujibu wa Jane, siku hizi 1,000 kama mama atakula lishe bora wakati wote na mtoto, huongeza uchumi wa nchi kwa maana ya kumwezesha kuzalisha pato la mwaka la (GDP) kwa asilimia 2-3.

"Siku hizi zikizingatiwa na wazazi kwa maana ya lishe bora kwa mama na mtoto akishazaliwa hadi kuadhimisha miaka miwili ya kuzaliwa, hupunguza uwezekano wa magonjwa ya muda mrefu (chronic diseases) na mzio (allergy)," anasema Jane.

### LISHE BORA NI IPI?

Mratibu huyo wa Programu wa PANITA, Jane Msagati, anafafanua kwamba, lishe ni hali ya mwili kupokea chakula chenye virutubisho vyote muhimu kwa ajili ya kuujenga, kuukinga na kuupa joto, hivyo kuuwezesha kufanya kazi vizuri.

Anataja virutubisho hivyo kuwa ni pamoja na protini, wanga, vitamini, madini, nyuzi nyuzi na maji.

Anasema matatizo makuu ya lishe nchini yamegawanyika katika makundi matatu: Upungufu au utapiamlo wa protini na wanga; upungufu au utapiamlo wa virutubisho vya vitamini na madini na hivi karibuni kumekuwa na utapiamlo utokanao na unene kupita kiasi.

"Lakini upungufu wa virutubisho vya vitamini na madini ndiyo unaoathiri zaidi sehemu kubwa ya jamii na waathirika wakubwa ni watoto walio katika umri wa chini ya miaka mitano na wanawake walio katika umri wa uzazi," anasema.

Jane anafafanua kwamba kwa kuwa mwili wa binadamu hauna uwezo wa kutengeneza virutubisho, chanzo kikuu cha virutubisho hivyo ni kutoka kwenye chakula na kwamba inatakiwa mtu, na hususani mtoto au mama mjamzito kula vyakula vinavyohitajiwa na mwili kila siku na siyo kile kinachomfurahisha kula.

Mtaalamu hiyo wa lishe anataja vyakula hivyo kuwa ni wanga kiasi kinachotakiwa (kama ugali, wali na maandazi), protini (nyama, maziwa, mayai na maharage) pamoja na vitamini na madini, vitu ambavyo vinapatikana zaidi kwenye matunda na mbogamboga.

Kwa mantiki hiyo, utaona kuwa Lucy ambaye ni mjamzito, hapati lishe inayotakiwa. Anaweza kuwa anapata wanga na protini lakini hali vya kutosha mbogamboga na matunda, vyakula ambavyo vitamsaidia kumuongezea vitamini na madini mbalimbalimbali.

Lakini mbaya zaidi, anakula ugali wa sembe ambao ni sawa na kula makapi, anakula chipsi na mayai au kuku wa kisasa ambao pia watalaamu wanasema ni chakula kisicho na virutubisho muhimu kwa binadamu.

### MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA SIKU 1000

Kwa mujibu wa Jane, kubwa la kuzingatia ni lishe bora ya mama mjamzito kama Lucy katika kipindi chote cha ujauzito na kufuatiwa na lishe bora ya mtoto tangu anapozaliwa hadi atakapofikisha umri wa miaka miwili na kuendelea.

Kadhalika, Jane anasena mtoto anatakiwa anyonye maziwa ya mama tu kwa miezi sita ya kwanza.

*Inaendelea uk. 18*



# Siku 1,000 za kujenga au kuharibu



*Inatoka uk. 17*

"Baada ya miezi sita, ni vyema mtoto alishwe vyakula vya ziada vyenye virutubisho vyote na wakati huo huo aendelee kunyonya maziwa ya mama yake," anasena Jane na kuongeza kwamba hii ya kunyonyesha mtoto inamfanya pia mtoto kuwa karibu zaidi na mama yake.

Jane anasema ni muhimu mama anayenyonyesha ahakikishe anapokwenda kwa daktari kama anaumwa amwambie mara moja bila hata kusubiri kuulizwa kuwa ananyonyesha ili asije akapewa dawa itakayokwenda hadi kwenye maziwa.

Anasema dawa kama hizo huweza kumfanya akakataa kunyonya baada ya kusikia harufu au ladha ambayo hakuzoea.

"Unajua mtoto anasikia sana harufu na ladha. Ndio maana mjamzito anatakiwa kuangalia sana anapoumwa kama dawa anayotaka kunywa inafaa kwa mama mjamzito au la. Kingine cha muhimu, mama anayenyonyesha hatakiwi kunywa pombe kwa sababu harufu yake ina kawaida ya kukimbilia kwenye maziwa. Hiyo pia inaweza kumfanya mtoto akatae kunyonya," anasema.

Anasema lingine la muhimu ni kuhakikisha kwamba mtoto anapata chanjo zote zilizoidhinishwa na serikali na pia kunakuwa na matumizi ya kutosha ya chumvi yenye madini joto.

Lingine analosisitiza Jane ni familia kumpa mama msaada wa kutosha kipindi chote cha kuanzia ujauzito na hadi kulea mtoto ikiwa ni pamoja na baba kuwa naye karibu, kula naye na kumsaidia shughuli.

"Mama anapokuwa katika miezi mitatu ya kwanza baada ya kushika mimba, yaani wakati mwili unapokuwa ukipambana kwa kudhani kuna kitu kibaya kimeingia mwilini, baba anatakiwa kuwaribu na mkewe hasa kipindi cha kula ili kumhimiza kula.

"Kama nilivyosema, muda wote wa ujauzito mama anapaswa kula lishe bora na inapendeza zaidi hata kabla ya kushika mimba mama ajiandae kwa lishe bora kwanza," anasema Jane.

Mtaalamu huyo wa lishe anasema ni muhimu baba ahusike kipindi chote cha mimba na ulezi wa mtoto ikiwa ni pamoja na kwenda kliniki, kuhakikisha kuna chakula cha kutosha, kutibu magonjwa na kumtia mama moyo wakati wote wa malezi ya mimba na mtoto.

Lingine la kuzingatia ni kuhakikisha vyakula vinaandaliwa katika mazingira safi na salama.

"Lingine ambalo wengi tunapuuzia ni kuboresha hali ya chakula katika kaya. Hili linaweza kufanywa kwa kutengeneza bustani ndogondogo kuzunguka nyumba au kama hakuna nafasi unaweza kufanya bustani ya makasha au viroba," anasema Jane.

Katika muktadha huo, Jane anashauri pia familia kufuga wanyama wadogo wadogo kama kuku, sungura pamoja na kukausha mboga mboga wakati wa masika na kuhifadhi kwa ajili ya kiangazi.

"Ni muihimu katika lishe ya mama na mtoto kuongeza vitu vya asili kama karanga kwenye mboga ili kuongeza virutubishi. Kadhalika tumia vizuri vyakula vinavyopatikana kirahisi katika mazingira yako ili kupunguza gharama, lakini la msingi ni kuhakikisha vyakula vina makundi yote ya lishe," anasema.



**MAKUNDI LISHE**

Makundi ya lishe na vyakula vyake ni pamoja na wanga unaopatikana katika vyakula kama mahindi, mtama, uwele, ulezi, ngano. Kundi lingine ni protini ambayo inaweza kupatikana katika maziwa, maharage, mbaazi, nyama na mayai.

Pia mwili unahitaji mafuta yanayoweza kupatikana katika karanga na ufuta; Vitamini inayopatikana katika mbogamboga zote na matunda na madini yanayopatikana zaidi katika mbogamboga.

**LISHE BORA NA ELIMU**

Kama ilivyodokezwa hapo juu, lishe katika siku 1,000 za mtoto ina nafasi kubwa katika kujenga afya yake ikiwa ni pamoja na ubongo wake.

Mwezi uliopita, matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yaliyotolewa na Baraza la Mitihani (Necta) yalionesha kwamba ufaulu umeshuka chini kwa asilimia 1.85 kwa kulinganisha na matokeo ya mwaka jana.

Pia ilielezwa kwamba somo la Hesabu liliendelea kuonekana gumu kwa watahiniwa wengi.

Kwa upande wa ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata watahiniwa wa shule, ililezwa kwamba waliopata daraja la Kwanza ni 9,816 sawa na asilimia 2.77, daraja la pili ni 31,986 sawa na asilimia 9.01, daraja la tatu ni 48,127 sawa na asilimia 13.56.

Waliopata daraja la nne ambalo kimsingi ni karibu na kufeli walikuwa 240,996, sawa na asilimia 67.91 na waliopata daraja la sifuri, yaani waliofeli kabisa walikuwa 113,489.

Sababu za kufeli kwa watoto wetu, mara nyingi kinachoangaliwa ni vitu kama waalimu wa kutosha, vitabu na hata mazingira ya kusomea. Lakini suala la udumavu wa akili wa watoto wengi haliangaliwi kama sababu ya wengi kutofanya vizuri.

Hili lingekuwa linafanyika pia ili kuwakumbusha wazazi na serikali kwa ujumla kuwekeza vya kutosha katika lishe bora ya watoto, hususani ndani ya siku 1,000.

**HALI ILIVYO NCHINI**

Takwimu za kitaifa juu upungufu wa virutubisho vya vitamini na madini zinaonesha kwamba katika vitamini A, watoto walioathirika asilimia 33 na akina mama asilimia 37.

Kuhusu upungufu wa damu (anemia), Jane Msagati anasema zaidi ya nusu ya watoto chini ya umri wa miaka mitano, yaani asilimia 59, wana upungufu wa damu na karibu asilimnia 41 ya akina mama wana upungufu wa damu pia.

Kuhusu upungufu wa madini joto, Jane anasema unachangia kwa kiasi kikubwa kudumaa kwa akili na kwamba mtoto akishapata hali hiyo huwa ni tatizo la kudumu.

Matatizo mengine ya ukosefu wa virutubisho mwilini ni kuharibika kwa mimba, kuzaa watoto wafu, utaahira, ulemavu, goita na udumavu ambapo zaidi ya watoto asilimia 42 wamedumaa.

Takwimu pia zinaonesha kwamba takribani watoto 130 walio chini ya umri wa miaka mitano hufa kila siku kutokana na matatizo ya lishe.

Na kwa mujibu wa takwimu hizo, zaidi ya wanawake 1600 hufa kila mwaka kutokana na matatizo mbalimbali yatokanayo na ukosefu wa damu wakati wa uzazi.

Ndio maana wazazi kama Lucy wanatakiwa kujitahidi kula lishe bora ambayo si ghali sana, kwani vitu kama fungu la mchicha au matembele kwa jiji kama Dar es Salaam halizidi Sh 500.

Wanaweza pia kula yai la kuku wa kienyeji ambalo ni wastani wa sh 500, kikombe cha maziwa pia hakizidi Sh 500 na chungwa la wastani halizidi Sh 200.

**ZINGATIA;** Makala hii ilishawahi kuchapishwa. Tumeirejea kutokana na umumu wake.

# Blinken atua Ukraine huku silaha za Marekani zikiwasili

**WASHINGTON, Marekani**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, amewasili Ukraine huku silaha kutoka kwenye fungu jipya la msaada wa Marekani, ukianza kuwasili mstari wa mbele.

Ziara yake inakuja wakati nchi hiyo ikijitahidi kuzuia uvamizi mkubwa wa Urusi karibu na mji wake wa pili kwa ukubwa wa Kharkiv.

Mwanadiplomasia Mkuu wa Marekani, anatarajiwa kukutana na Rais wa Ukraine,Volodymyr Zelensky na maafisa wengine.

Blinken atatoa ujumbe wa kutia moyo, maafisa wa Marekani wanasema.

Kuwasili kwa Waziri wa Mashauri ya nchi za kigeni jana, kunaadhimisha wiki tatu tangu Bunge la Congress la Marekani hatimaye likubali kifurushi kipya cha msaada cha $61bn (£49bn) kwa Ukraine.

Kabla ya Blinken kuwasili mjini Kyiv, Afisa Mkuu wa Marekani alisema silaha zinazofadhiliwa na Marekani ambazo sasa zinawasili kwenye mstari wa mbele, ni pamoja na viingilia ulinzi wa anga, mizinga na makombora ya masafa marefu ya kuongozwa na ATACMS.

"Tayari tumeanza kupeleka mizinga na ATACMS ya masafa marefu ambayo inaweza kuenea sehemu yoyote ya Ukraine, na pia uwezo mwingine wa ulinzi wa anga ambao unakusudiwa kukidhi mahitaji muhimu zaidi, haswa kwa kutazama shughuli za Urusi hivi sasa huko Kharkiv," afisa huyo alisema.

Blinken aliwasili kwa treni, akiingia Kyiv baada ya safari ya saa tisa kutoka mpaka wa Poland.

Aligusa Jumatatu katika mji wa Kusini-Mashariki mwa Poland wa Rzeszów, ambao uwanja wake wa ndege sasa ni kitovu kikuu cha vifaa kinacholeta vifaa vya ulinzi na misaada ya kibinadamu nchini Ukraine. BBC.



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken

# Vikosi vya Urusi vyatinga mji mkubwa wa pili Ukraine

**MOSCOW, Urusi**

URUSI imesema vikosi vyake vimeingia katika mji wa mpakani wa Kaskazini-Mashariki wa Vovchansk, karibu na mji wa pili kwa ukubwa nchini Ukraine Kharkiv.

Jeshi la Ukraine lilisema limewarudisha nyuma adui kutoka viunga vya kaskazini mwa mji huo na kuongeza kuwa lilikuwa na mafanikio ya kimbinu katika maeneo kadhaa.

Urusi imezidisha mashambulizi yake katika eneo hilo baada ya uvamizi wa ghafla wa Ijumaa iliyopita kuvuka mpaka na kutwaa takribani vijiji tisa na makazi katika moja ya mashambulizi muhimu zaidi ya ardhini tangu uvamizi wake dhidi ya Ukraine kuanza Februari, 2022.

Maelfu ya raia wamekimbia kuelekea Kharkiv. Kuna wasiwasi kati miongoni mwa makamanda wa Ukraine kuhusu nini kinaweza kutokea ikiwa wanajeshi wa Urusi wataingia ndani ya safu ya mizinga ya jiji.



Jeshi la Ukraine limesema kuwa Urusi imetuma vikosi muhimu katika mashambulizi yake ya hivi karibuni na limekiri kuwa wanajeshi wa Moscow wamepata mafanikio ya kimbinu.

Lakini katika taarifa ya jioni, jeshi lilisema Urusi imepoteza zaidi ya wanajeshi 100 tangu kuanza kwa siku hiyo na kuongeza kuwa vikosi vya Ukraine vinarejesha maeneo ya zamani.

Ilisema mapigano yalikuwa yakiendelea katika maeneo 12 na yameenea hadi kwenye makazi ya Staritsa, Magharibi mwa Vochansk.

Awali ilisema vikosi vya akiba vilikuwa vinahamishwa hadi Mkoa wa Kharkiv ili kuimarisha ulinzi wake. BBC.

# Msafirishaji wahamiaji haramu atiwa mbaroni

**BAGDAD, Iraq**

MMOJA wa wasafirishaji haramu wa watu barani Ulaya, amekamatwa nchini Iraq kufuatia uchunguzi wa BBC.

Barzan Majeed, alikamatwa huko Kurdistan ya Iraq Jumapili asubuhi,



Afisa Mkuu wa serikali alisema. Kwa miaka kadhaa, yeye na genge lake walijihusisha sana na biashara ya magendo ya watu katika boti na malori kwenye njia ya majini ya Uingereza.

BBC ilimtafuta Majeed maarufu kama Scorpion hadi mji wa Sulaymaniya, ambapo alisema alikuwa amesafirisha maelfu ya wahamiaji katika njia hiyo. "Labda elfu, labda 10,000. Sijui, idadi kamili," alisema.

Mkuu wa Serikali ya Mkoa wa Kurdistan alisema kuwa maafisa walitumia matokeo ya uchunguzi wa BBC kumpata Majeed.

"Alikamatwa saa moja asubuhi nje ya nyumba yake mara tu alipotoka nje bila mvutano makubwa," afisa huyo alisema na kuongeza:

"Sasa tunatathmini mashitaka dhidi yake, kisha tutajadiliana na polisi wa Ulaya na waendesha mashitaka ambao wanataka kumhoji na kumchukulia hatua."

Shirika la Kitaifa la Uhalifu la Uingereza (NCA), pia lilithibitisha kukamatwa kwake. BBC.

# Waandamanaji wa Israel wazuia malori ya misaada inayoelekea Gaza

**GAZA, Israel**

WAANDAMANAJI wa Israel wamezuia malori ya misaada iliyokuwa ikielekea Gaza siku ya Jumatatu, wakitupa vifurushi vya chakula barabarani na kufungua magunia ya nafaka katika eneo linalokaliwa la Ukingo wa Magharibi.

Malori hayo, ambayo yaliwekwa kwenye kizuizi cha Tarqumiya magharibi mwa Hebroni, yalitoka Jordan na yalikuwa yakielekea Ukanda wa Gaza, ambapo makumi ya maelfu ya Wapalestina wanakabiliwa na uhaba wa chakula na misaada.

Ikulu ya White House imelaani shambulizi hilo, ikilemea "uporaji" wamisafara ya misaada.

Kundi linaloripotiwa kuwa kwenye maandamano hayo lilisema walikuwa wakiandamana kupinga kuendelea kuzuiliwa kwa mateka wa Israel huko Gaza.

Picha ambazo hazijathibitishwa zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zilionesha waandamanaji wakiangusha masanduku kutoka kwenye lori na kuyakanyaga mara yalipoanguka.

Baadhi ya video zilionekana kuonesha magari yakichomwa moto baadaye jioni. BBC haijaweza kuthibitisha haya kwa uhuru.

Kulingana na ripoti katika vyombo vya habari vya Israel, kundi la wanaharakati la Tzav 9 lilihusika kuandaa maandamano hayo.

Ripoti za vyombo vya habari vya Israel zinaielezea kama kundi la mrengo wa kulia ambalo linatafuta kusitisha uhamishaji wa misaada ya kibinadamu hadi Gaza huku mateka wa Israel wakishikiliwa huko.

Muandamanaji mmoja aliliambia shirika la habari la AFP kuwa alikuwa katika kituo cha ukaguzi siku ya Jumatatu kwa sababu alisikia malori ya misaada yalikuwa "yakielekea mikononi mwa Hamas, ambao wanajaribu kuwaua wanajeshi wengine na raia wengine wa Israel"

Hana Giat, mwenye umri wa



miaka 33, alisema "hakuna chakula kinachopaswa kuingia Gaza" hadi mateka wa Israeli warudishwe wakiwa hai na wenye afya"

Katika taarifa iliyonukuliwa na gazeti la Jerusalem Post, Tzav 9 ilikataa baadhi ya vitendo vya waandamanaji, ikisema kuwa "vitendo vilifanywa leo ambavyo haviendani na maadili ya harakati zetu."

Iliongeza, hata hivyo, kwamba "kuzuia malori ni hatua ya ufanisi na ya vitendo ambapo tunapiga kelele kwamba hakuna msaada unaopita hadi mateka wa mwisho arudi"

Waandamanaji wanne, akiwemo mtoto mdogo, walikamatwa kwenyemaandamano hayo, kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa mawakili wao. BBC.

# Simulizi ya Juma Choka kimuziki


Juma Choka akiwajibika na zana zake

***Mwanamuziki mkongwe na mahiri katika kucharaza ngoma zinazoongoza muziki wa dansi 'drums', Juma Choka; anasimulia kiufupi historia yake ya maisha katika muziki huo kama alivyoombwa na Uelekeo. Pata uhondo!***

KWA jina naitwa Juma Choka ni Mwanamuziki wa dansi hapa Tanzania, historia yangu ya muziki inaanza mwishoni mwa miaka ya 1970 nilipoanza kujifunza upigaji wa drums. Historia ya maisha yangu kimuziki haiwezi kukamilika kama sitamtaja mwanamuziki nguli Mjusi Shemboza, nikiri huyu ndiye aliyenishika mkono kunipeleka kwa walimu wangu wa muziki.

Yeye akiwa mwanamuziki wa bendi ya Uda Jazz mara kadhaa alikuwa akinichukua kwenye mazoezi na maonyesho ya bendi yao ili kunikutanisha na mwanamuziki mwenzie ambaye alikuwa mpigaji mahiri wa drums kwa jina Said Chipembere.

Mjusi aliniusia sana niongeze bidii katika kupita njia za Said Chipembere, na kwa vile nilikuwa navutiwa na upigaji wake kweli sikufanya ajizi kujifunza upigaji wa drums.

Baada ya kuwa nimeanza kukomaa katika upigaji wa drums kwa mara ya kwanza kupanda jukwaani kama mwanamuziki ilikuwa mwaka 1979 nilipojiunga na Bendi ya Chamwino Jazz ya Dodoma, pale nilikaa kwa miaka mitatu kabla sijajiunga na bendi ya Urafiki Jazz iliyokuwa ikimilikiwa na kiwanda cha kutengeneza nguo, chini ya uongozi wa Mkongwe Juma Mrisho Feruzi maarufu kama Ngulimba wa Ngulimba.

Kama kawaida ya kazi ya muziki, kuhama kutoka bendi moja kwenda nyingine ni jambo la kawaida sana, nami sikuachwa nyuma na mkumbo huo, kwani baada ya muda nilijiunga na bendi ya Dar International wana Super Bomboka na mtindo wao wa Super Bomboka chini ya Marijani Rajab Doza. Nikiwa na bendi ya Dar International nilishiriki kurekodi nyimbo nyingi sana zilizovuma miongoni mwa hizo ni 'Masoud'.

Baada ya Dar International nilijiunga na bendi kadhaa hapa Dar es salaam zikiwemo Orchestra Mambo Bado chini ya uongozi wa Kalala Tshimanga Asossa na baadae mnamo mwaka 1985 nilijiunga na bendi maarufu ya Orchestra Marquis wana 'Zembwela'.

Hata hivyo, kwa sababu moja ama nyingine sikudumu sana na Marquis nikajiunga na bendi mpya ya OSS Safari Intimate Rhumba, hii ni bendi iliyokuwa ikimilikiwa na Hugo Kisima ambaye pia alikuwa akimiliki bendi ya Orchestra Safari Sound wana 'Dukuduku'.

Safari Intimate Rhumba ilikuwa ikiongozwa na Kikumbi Mwanza Mpango maarufu kama King Kiki.

Baada ya kufanya kazi na Safari Intimate Rhumba kwa muda mfupi nilijiunga na bendi ya Vijana Jazz wana Pambamoto chini ya Hemed Maneti Ulaya, hapa nimerekodi nyimbo nyingi sana tangu uhai wa Hemed Maneti na hata baada kufariki kwake mwaka 1990. Nimedumu na bendi ya Vijana Jazz kwa muda wa miaka minane mpaka mwaka 1995.

**SAFARI YA NAIROBI KENYA**

Baada ya kuachana na Vijana Jazz, mwaka 1995, safari ya kutafuta maisha na kuendelea kujifunza masuala ya muziki, ilinipeleka jijini Nairobi nchini Kenya. Huko nilikutana na Wanamuziki kadhaa Watanzania, miongoni mwao ni Abdallah Gama maarufu kama String Master, Musemba wa Minyugu na Rashid Sumuni.

Kwa kushirikiana na wenzangu hawa na wengine wenyeji wa Kenya nilifanikiwa kuanzisha bendi iliyokuwa ikiitwa Doreem Musica. Maskani ya bendi yetu pale mjini yalikuwa katika hotel iliyoitwa Benrose Motel, mbali na hoteli hiyo pia tulikuwa tukipiga katika kumbi mbalimbali kwa mikataba maalum.

Msomaji anaweza kujiuliza tuliwezaje kumiliki bendi katika nchi ya watu? Tulichokuwa tukifanya ilikuwa ni kutafuta mikataba na wamiliki wa kumbi za starehe na vilabu vya usiku ya kupiga muziki, baada ya kusaini mkataba unakuwa ni wajibu wetu kutafuta vyombo hasa vya kukodi, ambavyo jijini Nairobi ilikuwa ni biashara ya watu.

Miongoni mwa Wakenya waliokuwa wakifanya biashara ya kukodisha vyombo vya muziki aliitwa Philip, kupitia huyu mwamba ndio nilipata vyombo vya kuendeshea bendi ya Doreem Musica ambayo miongoni mwa wanamuziki waliokuwemo ni mapacha raia wa Congo DRC, Kasaloo Kyanga na Kyanga Songa ambao kwa sasa wameshatangulia mbele ya haki.

Hawa wamewahi kutamba na bendi kadhaa Tanzania zikiwemo Super Matimila, Orchestra Marquis, Ngorongoro Heroes na Tancut Almasi.

Masikitiko makubwa ni kuwa Doreem Musica haikuweza kutamba katika soko la muziki Nairobi na Kenya kwa ujumla sababu kubwa ikiwa ni tabia ya ulevi wa kupindukia ya hawa ndugu mapacha Kyanga Songa na Kasaloo Kyanga. Hivyo basi Doreem Musica ilisambaratika na kila mwanamuziki akalazimika kushika hamsini zake kusaka malisho kwa namna alivyoweza.

***Itaendelea Jumatano ijayo.***


Juma Choka

# Sauti za Afrika katika muziki wa hip hop


Rosa Ree


Nasty C


50 Cent

Bill Nass


Sarkodie

**Na Valensi Mbaga**

TANGU hip-hop ilipoingia katika bara la Afrika na kusababisha mabadiliko ya kitamaduni katika miaka ya 1980 na 1990, aina hiyo imeendelea kubadilika, na kuzaa vizazi vya rappers wenye vipawavi kubwa zaidi.

Kuanzia Asaka Drill nchini Ghana hadi Bongo Flava nchini Tanzania, marapa mahiri kote barani Afrika wanabuni sauti nyingi za kiasili, wakionyesha ubunifu usio na kikomo na mbinu ya kipekee ambayo imeweka rap ya Kiafrika kwenye ramani. Wafuatao ni wasanii wa kizazi cha hivi karibuni cha rappers ambao wamefanikiwa kusonga mbele zaidi na kuweka majina yao katika historia.

### Sarkodie

Huwezi kuwatosheleza wapenzi wa rap bila kusikiliza nyimbo za Sarkodie tangu alipopata umaarufu. Rapa huyo wa Ghana ni hodari sana katika upangaji wa mashari na ana mtiririko usio na kifani ambao unazipa rekodi zake mguso wa kipekee.

Sarkodie ametawala kwa zaidi ya muongo mmoja, akifungua njia kwa vijana wengine chipukizi na kuchangia katika kuenea duniani kote kwa rap ya Kiafrika.

Amefanya kazi na wasanii mbalimbali barani Afrika, na kuimarisha hadhi yake kama kiongozi mkubwa wa rap Afrika.

### Nasty C

Rapa huyo mzaliwa wa Afrika Kusini alikuja kujulikana mwaka wa 2016 alipotoa wimbo maarufu zaidi wa "Juice Back," ambao ulipata remix na Davido na Cassper Nyovest.

Nasty C anachukuliwa kama aina maalum katika hip-hop ya Kiafrika, akiwa ameshirikiana na waigizaji maarufu kama French Montana na ASAP Ferg, na kuwa katika usukani wa utandawazi wa muziki wa Kiafrika.

Akiwa na albamu tatu za studio na zaidi ya miito milioni 100 ya kazi kwa jina lake, rapper huyo mwenye umri wa miaka 26 ni mmoja wa wasanii maarufu wa rap wa Kiafrika.

### Blaqbonez

Sio rappers wengi hufanya kama Blaqbonez. Mwanamuziki huyo anayejiita "Best Rapper in Africa" amejidhihirisha kuwa mtu wa kutegemewa, na kujikusanyia mashabiki wengi kutokana na mbinu yake ya ubunifu katika kutafuta masoko.

Blaqbonez alivamia tasnia hiyo kwa mtiririko na maandishi yake tofauti mnamo 2018 na albamu yake iliyosifiwa sana, Bad Boy Blaq. Akitumia vipengele vya Afropop katika nyimbo zake za rap, ametoa rekodi ambazo zimemgusa sana wafuasi wengi wanaosikiliza kazi zake.

### Khaligraph Jones

Ingawa Khaligraph Jones alianza kurap tangu siku zake za shule ya sekondari, ilikuwa hadi 2008 alipotoa "Maneno na Picha" ndipo alianza rasmi kazi yake kama rapper.

Mnamo mwaka wa 2018, Khaligraph Jones alitoa albamu yake ya kwanza ya Testimony 1990, ambayo ilimfanya aingie kwenye mkondo wa rap ya Afrka.

Aliteuliwa pamoja na Nasty C kwa Tuzo za BET katika kitengo cha Mtiririko Bora wa Kimataifa mwaka wa 2020. Yeye ni mmoja wa wasanii wachache wa rapa kutoka Afrika Mashariki wanaofanya vizuri kwenye eneo la rap nchini Kenya na kimataifa.

### Rosa Ree

Haikuwashangaza wengi walipomwona Rosa Ree akishiriki katika kipengele cha BET Hip hop Cypher 2020, pamoja na Kwesi Arthur na Elizabeth Ventura.

Tangu alipoanza kurap mwaka 2016, alipotoa wimbo wa "One Time", rapper huyo wa Tanzania hajafunga breki. Alitoa albamu yake ya kwanza ya Goddess mnamo 2022, akizidi kuchanua mbawa zake zake katika tasnia inayokua kwa kasi ambayo inatawaliwa zaidi na rappers wa kiume.

### AKA

AKA alitambulishwa kwa umati mkubwa alipotoa wimbo wa "Victory Lap" mnamo 2011, wimbo ulioongoza chati ambao ulitangulia albamu yake ya kwanza ya Altar Ego.

AKA anashikilia rekodi ya kuwa rapper wa kwanza kutoka Afrika Kusini kuwa na albamu iliyouza kwa kiwango cha platinam. Diskografia yake imejaa rekodi na albamu zilizovuka mipaka.

Hadi kifo chake cha kusikitisha, rapa huyo alikuwa nyota anayeng'aa katika tasnia ya rap, akihamasisha kizazi kipya cha rappers wa Kiafrika.

### Bill Nass

Muda mfupi baada ya Bill Nass kuachia wimbo wake wa kwanza "Raha" mwaka 2015 aliteuliwa kuwa Msanii Mpya Bora katika Tuzo za Kilimanjaro Tanzania Music Awards (KTMA).

Rapa huyo amekuwa kwenye ubora tangu wakati huo, akiipeleka muziki wa hip-hop nchini Tanzania katika hali ya juu zaidi. Anatambulika kama mojawapo ya sauti za kipekee zinazochangia uenezaji wa sauti za Kiafrika.

### Femi One

Baada ya kucheza pamoja na wasanii wengine wa kike kwenye remix ya wimbo wa King Kaka "Ligi Soo" na kusainiwa na lebo yake ya rekodi, Femi One one ameendelea kujiweka kando katika tasnia ya muziki nchini Kenya kutokana na mashairi yake yamezidi kumpaisha katka viwango vya juu zaidi.

Alitoa albamu yake ya kwanza ya Greatness mwaka wa 2021, akirap hasa kwa Kiswahili na Sheng, na kuimarisha nafasi yake kama sauti inayoongoza Afrika Mashariki.

# Pamba itatukumbusha enzi ya 'TP Lindanda'


Kikosi cha Pamba Jiji


Marehemu Magongo


Khalfan Ngassa


Nteze John

**Na Hamid Yassin**

WIKI iliyopita tulishuhudia mabingwa wa zamani wa Tanzania Pamba ikirejea kwenye Ligi Kuu ya soka la hapa nchini. Hii timu ina historia ya kusisimua tangu enzi za miaka ya sabini hadi ilipoanza kupotea taratibu baada ya kutemwa na waliokuwa wanaimiliki Mamlaka ya Pamba.

Kuzorota na hatimaye kupotea kwa miaka mingi kwa timu ya Pamba ni matokeo ya Mashirika ya Umma kujiweka pembeni katika kuwekeza kwenye michezo mwishoni mwa miaka ya 1990 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Ziko wapi zile timu za Biashara kwenye kila Mkoa? Ziko wapi zile za Mashirika kama Pilsner na Ndovu zilizomilikiwa na Kiwanda cha Bia nchini (TBL)? Unaikumbuka timu ya Sigara? Wawekezaji wa kigeni ndiyo waliozipoteza timu hizo na nyingine nyingi zilizotamba miaka ile.

Huo ndiyo ukweli, kujiweka pembeni katika michezo kwa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kulikuwa ndiyo chanzo kwa kupotea kwa timu nyingi zilizotamba miaka hiyo kama vile CDA ya Dodoma, Ushirika Moshi, RTC Kagera, Biashara Mwanza, RTC Kigoma na nyingine kadhaa.

**PAMBA FC**

Pamba ilikuwa na vizazi kama vitatu hivi vya wachezaji hodari na mahiri walioibeba timu hiyo mabegani mwao hadi kufikia kuporomoka baada ya kutemwa na Bodi ya Pamba iliyokuwa inatoa huduma zote muhimu kwa timu hii mwishoni mwa miaka ya tisini.

Kizazi cha kwanza kilichotingisha sana ni kile cha miaka ya 70 mwishoni hadi themanini mwanzoni, baadhi ya wachezaji wale ni pamoja na akina Juma Mhina, Issa Melloo, Joram Mwakatika, Ibrahim Magongo, Abbas Magongo, Halid Bitebo ' Zembwela' Abdallah Bori, Venance Kazungu, Richard Hiza, Mwinda Ramadhani 'Maajabu', Rafael Paul na wengine kadhaa.

Kizazi hiki kilitingisha sana kwenye Ligi Daraja la Kwanza wakati ule ikiwa ndiyo ligi ya ngazi ya juu zaidi ingawa hakikuwahi kutwaa ubingwa wowote wa nchi hii. Lakini hayo hapo juu ni majina makubwa ya nyota waliotamba vilivyo kwenye soka la nchi hii.

Timu ikaanza kubadilishwa taratibu hadi kikaja kizazi kingine cha hatari pia, Madata Lubigisa ambaye alikuwa anawekwa benchi na Juma Mhina akaanza kuchomoka kwa kasi, hiki pia unaweza kukiita kizazi cha akina Khalfan Ngassa, Rajabu Risasi, Beya Simba, David Mwakalebela, Shabaan Makinka, Dan Mhoja, Rwemao Mkama, James Washokera, Hamza Mponda, John Makelele, Kitwana Suleiman, George Gole, Rashidi Abdallah Magongo na wengine kadhaa.

Kumbuka kipindi chote hiki kiboko mkubwa wa Pamba katika soka la Mwanza ilikuwa timu Coop United iliyokuwa inamilikiwa na Chama cha Ushirika cha Nyanza mkoani humo.

Coop United iliyokuwa chini ya kocha marehemu Muhsini Mafutah ( kaka yake Juma Amir Pele wa Mwanza), ilikuwa na mastaa hodari kama vile Juma Amir, Hussein Masha, George Masatu, Msonga Rashidi, Mao Mkami 'Ball dancer', Kingsley Malilo, pia walikuwa na kipa wao hodari Karume (Kenge). Hapa Pamba katika zile mechi za kirafiki na maalumu za kimkoa alikuwa anapigwa kama amesimama.

Pamba ilikuwa inawataka sana nyota wa Coop lakini kikwazo kikubwa ilikuwa kocha wao Maftah, wachezaji wote hawa aliwaandaa na kuwafundisha yeye tangu wakiwa wadogo, hivyo walimtii sana.

Baadaye Pamba wakaona isiwe taabu kwenye udhia penyeza Rupia, kuelekea miaka ya mwishoni ya themanini, wakaamua kumchukua huyu kocha Maftah na wachezaji wake wote nyota akina Mao, Masha, Masatu, Msonga, Juma Amir kwenda kuanzisha kizazi cha tatu hatari cha Pamba chini ya Bodi ya Pamba iliyokuwa inaongozwa na mwanamichezo maarufu, marehemu George Mpondela 'Castro'.

Huyu marehemu Mpondela baada kutoka Mamlaka ya Pamba alikwenda kuwa Katibu Mkuu wa Yanga na ndipo alipobandikwa jina la 'Castro' kutokana na misimamo yake mikali dhidi ya waliokuwa wafadhili wa Yanga wenye asili ya Kihindi marehemu Abbas Gulamali na wenzake kina marehemu Mohamed Vilani, Rameshi Patwa na wengineo.

Baada ya kuwanasa akina Masha na wenzake, Pamba iliongeza wachezaji kutoka timu nyingine za Mwanza na Mkoa wa jirani wa Shinyanga kama vile Fumo Fellician, Ntenze John Rungu, Nicco Bambaga kwa kushirikiana na baadhi ya wachezaji waandamizi waliowakuta, Pamba ikawa timu yakutoa dozi kali kwa kila aliyekatiza mbele yake.

Hapa ndipo jina la TP Lindanda lilipochomoza kupitia mtangazaji nguli wa RTD wakati huo marehemu, Dominic Chilambo!

Bado nakumbuka jinsi timu ya Pamba FC maarufu kama Wana-TP Lindanda iliyokuwa na wachezaji wazalendo watupu walipoifunga timu ya Anse-aux- Pins FC ya Seychelles jumla bao 17-1.

Hiyo ilikuwa kwenye michuano ya Kombe la Washindi mwaka 1990, baada ya kushinda ugenini bao 5-0 na kuja kumalizia kazi kwenye mechi ya marudiano pale CCM Kirumba kwa kuishindilia timu ile bao 12-1.

Ushindi ule wa Pamba katika mechi iliyotangazwa na marehemu Chilambo, ndiyo rekodi kwa timu zote za Tanzania na Afrika kwa ujumla kwa ushindi mkubwa hadi hivi sasa!

Je, hii Pamba ambayo sasa imebadilishwa jina kutoka Pamba FC iliyokuwa chini ya Bodi ya Pamba hadi sasa kuitwa Pamba Jiji kufuatia aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amosi Makala kuikabidhi kwa Jiji hilo la milima, itaturudisha enzi zile za TP Lindanda ama imekuja Ligi Kuu ya NBC kusalimu kisha kurejea kule ilipozoea kwenye Championship? Ni suala la kusubiri!

**Kwa maoni na ushauri; 0784 122 020 ama 0768 888 787.**

# Pep Guardiola afichua nondo zake muhimu



**Na Valensi Mbaga**

KOCHA mkuu wa klabu ya Manchester City, Pep Guardiola amesema Manchester United na Chelsea zitakuwa na changamoto kuishusha Manchester City na Arsenal kuwania taji la Ligi ya Premia ikiwa tu wataendelea kuamini kuwa mafanikio yatatokana na matumizi makubwa ya pesa kwenye kusajili.

Meneja wa City anakataa dhana kwamba mafanikio ya timu yake yanatokana fedha na kudai kuwa, ingekuwa pesa ndio sababu pekee basi City wasingepata mafanikio waliyonayo hivi sasa.

City wameshinda taji la kihistoria na la nne mfululizo la Ligi Kuu ya England, na wameshinda mara tatu na kuwa klabu ya kwanza kufanya hivyo kwa kuchukua vikombe vyote vitatu kwa pamoja. Ikiwa ni Kombe la FA mara mbili katika misimu mfululizo na UEFA mara moja.

Inaonekana kuwa ni hali ya kutokuepukika juu ya mafanikio yao baada ya kucheza mechi 21 bila kushindwa ambayo imejumuisha sare nne pekee.

"Kama ingekuwa sababu ni pesa, basi Manchester United walipaswa kushinda mataji yote, au Chelsea mataji yote, au pengine Arsenal mataji yote. Wanatumia pesa nyingi katika miaka mitano iliyopita kama sisi. Wanapaswa kuwepo mbali sana," amedai Guardiola na kuongeza.

"Kwa sababu hiyo basi pengine Girona haipaswi kuwa kwenye Ligi ya Mabingwa msimu ujao na Leicester inapaswa kushinda Ligi ya kuu ya EPL."

City inakadiriwa kuwa katika nafasi ya saba katika orodha ya jumla ya pesa zilizotumika kwenye Ligi Kuu England katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, chini ya nusu ya Chelsea, Manchester United na Arsenal lakini pia ikifuatiwa na Tottenham, Newcastle na Aston Villa.

Sababu kubwa iliyofanya idadi yao kushuka hadi Paundi milioni 259 imekuwa uwezo wao wa kuuza wachezaji kama vile Gabriel Jesus, Oleksandr Zinchenko, Riyad Mahrez, Aymeric Laporte na Cole Palmer kwa kiasi kikubwa.

Hakuna hata mmoja wa wachezaji hawa ambaye angechukuliwa kuwa chaguo la kwanza la moja kwa moja na bila wao wanakaribia kuwa timu ya kwanza tangu ligi ya England ilipoundwa mnamo 1888 kushinda Ligi Kuu misimu minne mfululizo.

"Hakuna timu iliyowahi kuchukua makombe kama ilivyo City na hali Hiyo inaonyesha jinsi ilivyo ngumu. Liverpool katika miaka ya 80, United ya Sir Alex Ferguson katika miaka ya 90. Chelsea wakiwa na Roman Abramovich na Jose Mourinho, Arsenal wakiwa na Arsene Wenger hawakufanya hivyo." Aliongeza

Guardiola anasema wazo hilo halikuwa mbele ya vichwa vya City na siri pekee ni kutengeneza timu yenye wachezaji wenye utayari wa kupambania timu haijalishi ukubwa wa majina yao au ubora woa pia.

# Minong'ono ya usajili Ulaya

## Liverpool wamtolea macho Gordon



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Liverpool wanataka kumsajili winga wa Newcastle, Antony Gordon. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uingereza, 23, amefurahia msimu mzuri wa kwanza huko St James Park na anatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi cha Gareth Southgate katika michuano ya Uropa msimu huu.

Ubora huo thabiti akiwa chini ya mwalimu Eddie Howe umevutia kitengo cha skauti cha Liverpool na kuhitaji huduma yake msimu ujao huku wakimkosa kocha wao Jurgen Klopp.

## Diaz akataa ofa PSG



**LIVERPOOL, England**

NYOTA wa Liverpool Luis Diaz amepuuza mapendekezo ya kuondoka majira ya joto kwa kusisitiza kuwa anaamini mafanikio makubwa yanakuja kwa Reds.

Diaz alijiunga kutoka Porto Januari 2022 na ana kandarasi Anfield hadi 2027, lakini kumekuwa na mazungumzo ya kuhama kabla ya hapo na Paris Saint-Germain miongoni mwatimu zinazohusishwa kumuhitaji.

## Saudia waweka kambi kwa Casemiro

**RIYADH, Saudi Arabia**

KLABU mbalimbali za Saudi Pro League vinashinikiza kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United Casemiro wakati dirisha la uhamisho litakapofunguliwa mwezi ujao.

Kulingana na vyanzo vya habari hadi wachezaji 10 wa Ligi Kuu ya England wanatarajiwa kutimkia Saudia msimu huu wa joto huku klabu ya Al-Nassr yenye nyota kama Cristiano Ronaldo, Aymeric Laporte na Sadio Mané, wanaohusishwa zaidi kujumuishwa na Casemiro.

Wawakilishi wa Mbrazil huyo tayari wanafahamika kuwa walifanya mazungumzo na vilabu vya Saudia Pro League. United wako tayari kumuuza na wangependa makubaliano yoyote yakubaliwe mwanzoni mwa dirisha lakini hawatamsukuma Casemiro kutokucheza mechi zilizosalia.



## Madrid wamvalia njuga Trent - Alexander Arnold

**MADRID, Hispania**



MTAALAMU wa masuala ya uhamisho wa wachezaji Fabrizio Romano amethibitisha kwamba Real Madrid wanatafuta kumsajili Trent Alexander-Arnold kutoka Liverpool huku hali ya kandarasi ya beki huyo ikiwa matatani.

Alexander-Arnold, Mohamed Salah na Virgil van Dijk wote wamehusishwa na uhamisho wa kwenda kwingine huku kandarasi zao zikitarajiwa kuisha msimu wa joto wa 2025. Kumekuwa na uvumi kwamba Real Madrid wanataka kumsajili Alexander-Arnold ili kuziba pengo la mkongwe Dani Carvajal kwani Mwingereza huyo ni mmoja wa wachezaji bora katika nafasi yake katika soka la dunia kwa sasa.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Mei 15 - 21, 2024 |

## Mazembe yawatembelea Wananchi Jangwani

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa TP Mazembe umetembelea Makao Makuu ya klabu ya Yanga SC na kutembezwa maeneo mbalimbali ya klabu hiyo.

Uongozi huo chini ya Mtendaji wake Mkuu (CEO), Freddie Kitenge ulikwenda Makao ya klabu hiyo na kukutana




na CEO wa Yanga, Andrie Mtine, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ally Kamwe pamoja na Stafu wengine wa Yanga SC waliowatembeza viongozi hao wa Mazembe.

Wiki iliyopita Rais wa Yanga SC, Mhandisi Hersi Said alikuwa nchini Congo DR na alikutana na Rais wa TP Mazembe, Moise Katumbi.

# Simba SC yaibomoa tena Coastal Union

## ● Kibu bado hajasaini kwa Wekundu wa Msimbazi

**Na Mwandishi Wetu**


BAADA ya wiki iliyopita kufanikiwa kumsainisha beki mahiri wa Coastal Union, Lameck Elias Lawi, Klabu ya Simba imewabomoa tena 'Wagosi wa Kaya' kwa kuwachukua wachezaji wake wengine wawili kipa, Ley Ngumba Matampi na beki wa kushoto, Miraji Abdallah.


Habari za uhakika kutoka ndani ya klabu hiyo ya Simba zimebainisha kuwa wako kwenye hatua za mwisho za kuapata saini za wachezaji hao tegemeo wa Coastal Union.

Matampi raia wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo aliyefanya vizuri msimu huu kwa kuing'arisha Coastal vya kutosha, imeelezwa kwamba, anakwenda Simba kuchukua nafasi ya kipa Mmorocco Ayoub Lakred ambaye amegoma kuongeza mkataba na Wekundu wa Msimbazi hao.

Matampi ambaye ameibeba Coastal mgongoni mwake kwenye mechi nyingi msimu huu, hajaruhusu wavu wake kutikiswa katika mechi 12 msimu huu akiwa amezidiwa na kipa wa Yanga tu, Djigui Diarra mwenye 'Clean Sheets' 13 hadi sasa.

Naye beki Miraji imepashwa kuwa, anakwenda Simba kusaidiana na mkongwe Mohamed Hussein ambaye kwa misimu kadhaa amecheza mechi nyingi mfululizo kutokana na kukosa masaidi sahihi.







Miraji ambaye naye amekuwa na msimu mzuri, ni matunda ya timu za vijana za Coastal Union ambao nao wamekuwa na utamaduni wa kuibua vipaji vingi kila msimu ingawa hawaimbwi sana.

Mbali ya wachezaji hao wazawa, pia Simba inaendelea na zoezi la kusaka nyota wa kigeni wa kuwasainisha na habari za hivi punde kutoka ndani ya timu hiyo zimebainisha kuwa wako katika hatua za mwisho za kumsanisha kiungo mkabaji, Mghana Foday Trawally anayecheza soka la kulipwa nchini Uturuki.

Wakati huo huo, Carlos Sylivester ambaye ni Meneja wa kiungo mshambuliaji wa klabu ya Simba, Kibu Denis ameweka wazi kwamba mchezaji wake huyo bado hajasaini mkataba mpya na klabu yake hiyo.

Carlos maarufu kama 'Mastermind' amepasha kuwa, ni kweli wapo kwenye mazungumzo na Simba ambayo yanaelekea ukingoni, lakini Kibu bado hajasaini mktaba wowote ule kama inavyovumishwa kwenye vyombo vya habari.

"Hata mimi naziona hizo taarifa kwenye vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii zikidai eti Kibu ameshamalizana na Simba kwa kusaini mkataba wa miaka miwili, siyo kweli, mimi ndiye Meneja wake ninayesimamia masuala yake yote ya soka," amesisitiza Carlos 'Mastermind'.

# Mwamnyeto: Siondoki Yanga ng'o

## ● Job, Kibwana waisikitikia Mtibwa Sugar



**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa mabingwa wa soka nchini Yanga, Bakari Mwamnyeto amesema kuwa, kamwe hafikirii kuihama klabu hiyo labda ikitokea Wananchi wenyewe wamuache.

Mwamnyeto alitoa kauli hiyo juzi mara baada ya Yanga kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC kwa kuichapa Mtibwa Sugar goli 1-3 na kufikisha alama 71 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote ile.

Beki huyo wa kati amefunguka hayo kwa mara ya kwanza baada ya kuenea kwa tetesi za kuhitajika na Simba Sc ambapo amesisitiza hawezi kuondoka Yanga labda wamfukuze!

Nao mabeki Dickson Job na Kibwana Shomari wamesema wanasikitishwa na hali inayopitia timu iliyowaibua katika Ulimwengu wa soka ya Mtibwa Sugar ya kupigania kutoshuka daraja kwa mwaka wa nne sasa mfululizo.

Job kwanza ameweka bayana kuwa, ana furaha kubwa ya kutwaa ubingwa wa tatu mfululizo akiwa na Yanga pamoja na timu yake hiyo kuchangia kuichimbia 'kaburi' Mtibwa Sugar la kushuka daraja.

"Naisikitikia Mtibwa Sugar katika hali hii wanayopitia, lakini lazima niwe muwazi, nina furaha kubwa kushinda leo na kutwaa ubingwa kwani hii ni kazi yangu," amebainisha Job.

Naye Kibwana ambaye kama Job ameptia Mtibwa Sugar kuanzia timu za vijana hadi ile ya wakubwa, amepasha kwamba ana imani timu yake hiyo itavuka huu mtihani wa kutoshuka daraja unaowakabili.

Kibwana amewataka Mtibwa kupigana kwa nguvu zao zote kushinda mechi tatu zilizobaki waone kama wanaweza kujiokoa na kushuka daraja.

